# *Na Uzao Wako Utamiliki Mlango Wa Adui Zake*

Na tuendelee kusimama, na kuinamisha tu vichwa vyetu kwa ajili ya maombi.

2 Baba yetu wa Mbinguni mwenye Neema, ni mara nyingine tena tunakukaribia Wewe, tukiomba msamaha wa dhambi zetu na makosa yetu, na kuomba ya kwamba utaturehemu, Baba. Tungeomba, Bwana, ya kwamba utusamehe makosa yetu yote, utuongoze katika njia za Nuru na Uzima.

3 Na utufanye, Bwana, kukolea chumvi sana hata wengine wangetamani kuwa Wakristo, wale tunaowasiliana nao, tunajua ya kwamba chumvi ina ladha inapoonjwa. Basi Baba, tunaomba ya kwamba utatufanya sisi nguvu za chumvi, na jalia tuwe na shauku sana ya kuwasiliana na ulimwengu wa nje unaokufa, ili kwamba iwe ni ladha kwao. Tunaambiwa kwamba sisi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote, na, Baba, tunaomba ya kwamba maisha yetu yatakuwa hivyo, tunapokiri kuwa na tukio hili kuu la Pentekoste, ya kwamba yatakuwa yenye—yenye *chumvi* sana kwa ulimwengu, hata watatamani kuwa hivyo pia.

4 Tupe Roho Wako Mtakatifu, Bwana, tupate kuuonyesha ulimwengu, ya kwamba imani yetu katika Mwokozi wetu imethibitishwa, kwamba Yeye hajafa, bali anaishi pamoja nasi siku baada ya siku, akituongoza na kutuelekeza, akitulisha, tukitembea karibu na maji matulivu na malisho ya kijani kibichi yenye kivuli.

5 Tunaomba ya kwamba utatubariki usiku wa leo katika Neno. Waponye wagonjwa na wanaoteseka, waokoe waliopotea. Jitwalie utukufu kwa Jina Lako kuu, kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lako, Yesu Kristo. Amina.

Mnaweza kuketi.

6 Kwa kweli, tunayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kurudi tena usiku wa leo, hapa kanisani, kuwahudumia tena watu Neno. Na hii imekuwa ni siku kuu. Nina furaha sana kukutana na Wakristo, kukutana na watu halisi, waliozaliwa mara ya pili. Natumaini hamdhani ya kwamba mimi, nikielezea na kusema mambo ninayosema, kwamba nafikiri kwamba California ina wenye dhambi wote, wako kote ulimwenguni. Nami nina. . .Jana jioni nilipokuwa nikikaribia, nilikuwa huko chini mjini wakati wa alasiri, nami nikaona ya kwamba baadhi ya watu, jinsi walivyokuwa wakitenda, kama tu wanavyofanya katika sehemu zingine za ulimwengu.

7 Nami niliingia jana usiku, na maskini msichana mzuri kuliko wote, kutoka jukwaani hapa, kutoka kwenye kwaya, naamini ndivyo ilivyokuwa, akarudi pale. Alikuwa ni Mkanada, maskini mama mzuri sana, aliyeonekana safi, na mama halisi tu, halisi sana, natumaini Rebekah wangu atakuwa hivyo atakapofikia umri wake, msichana wa Kanada. Halafu basi, usiku wa leo, nikiingia, huko nje kando ya ukuta alisimama ma—maskini mama mmoja, nikisimama huko nje, wakati mwanangu, na binti mkwe wangu walipokuja huku, nami, kutoka Arkansas, wakingojea huko nje kwenye baridi wapate tu kuniamkua, kasema alikuwa amekumbuka wakati nilipokuwa Hot Springs miaka mingi, mingi iliyopita, ile familia ya Humbard. Na kuwaona tu watu kama hao, inafanya tu maisha yastahili kuishiwa.

8 Mwajua, tu—tunaishi tupate kutumika, na kufanya tuwezayo kwa ajili ya watu hao, na kujaribu kuwasaidia wengine ambao labda hawajui furaha ya kuishi maisha hayo. Baadhi ya watu wanafikiri ya kwamba unapokuwa Mkristo kwamba inahi-. . . inaondoa tu furaha yote maishani, ni vinginevyo tu. Ni—nimeishi kwa njia zote mbili, hii ni miaka thelathini na moja nimekuwa nikihubiri, nami nimekuwa . . . Nisingebadilisha maisha haya na chochote hata kama hakukuwa na Mbingu yoyote ya kuiendea mwishoni mwake, ingawa hakukuwako na Yesu yeyote wa kuona. Nina furaha zaidi kuishi namna hii kuliko vile mimi, siku moja, kuliko vile ningeishi kwa miaka kumi kwa njia nyingine yoyote, kama kusingekuwako na kitu baadaye.

9 Lakini hilo kweli linatoka moyoni mwangu, kama—kama ndugu yenu na mtumishi wa Mungu. Kuna amani kuu sana na utoshelevu, ukijua ya kwamba unapolala kama hutaamka tena, inaleta tofauti gani? Unaona? Ume—ume—umeokoka, ile—ile nanga inayoshikilia ndani ya pazia mahali fulani huko nje, kitu ambacho kinatwambia kwamba mazuri yako tu Ng'ambo ya pili.

10 Billy aliniambia jana usiku nilipoondoka, akasema, "Baba, unafikiri ungeweza kujimudu wakati mwingine utoke saa tatu?"

Nikasema, "Natumaini hivyo, wakati fulani." Lakini mimi . . . Ninyi ni watu wazuri sana kuzungumzia, nanyi . . . hakuna mahali pa kusimamia.

Naye akasema, "Vema, jambo la kwanza, ulizungumza yapata dakika thelathini kabla hujaanza mahubiri yako."

11 Nikasema, "Sasa, Billy, nitaninii, sitafanya hivyo usiku wa leo, Ni—nitaanza kuhubiri mara moja upesi sana, ili niweze kuwaachilia watu waondoke."

12 Tuna, bado juma zima; halafu inatubidi kutoka hapa kisha tuingie Visalia; na moja kwa moja kutoka huko hadi Ohio, kurudi kwenye theluji; na huko chini Virginia, ambako nafikiri wana inchi kumi na saba za theluji mle ndani sasa; kisha turudi

Illinois, Bloomington, huko Chicago; na halafu huko juu kabisa kaskazini mwa British Columbia, ambako theluji inaanguka kweli; halafu basi, natumaini, Bwana akipenda, wakati fulani katika msimu huu wa kiangazi, ku—kwenda ng'ambo tena, kwa sababu huko ndiko moyo wangu uliko. Hiyo ni kweli. Wewe ungefanya hivyo, pia.

Unasema, "Vema, wewe hutupendi."

13 Naam, ninawapenda, lakini tayari mmetiwa nanga katika Kristo, nao hao watu kule, wakiona njaa sana na kiu. Na sasa, kama nilikuwa nikiwafanyia kazi, nami ningeweza kuchuma, nilikuwa nikichuma maforosadi, upande mmoja wa barabara *hapa*, ningeweza kuchuma galoni hamsini kwa siku, upande *huu* wa barabara, ningeweza kuchuma kwati mbili kwa siku. Sasa, inanipasa kushughulikia upande gani? Bila shaka. Mnajua ninalomaanisha.

14 Lakini jambo moja kuhusu kuwa na mikutano hapa, Wamarekani wana pesa, nao ndio wanaopaswa kudhamini. Hao watu hata hawawezi kula kule ila kile. . .na ni kubaya sana, kamwe msingetambua kile lilicho.

15 Halitaugusa moyo wako mpaka usimame barabarani wakati fulani, ukihubiri, na kumwona maskini mama na mtoto wake mchanga, huku tumbo lake limevimba juu *hivi*, akifa kwa njaa, naye anajaribu kukupa huyo mtoto mchanga, anajua yeye atakufa, pia, akifa kwa njaa. Vema, vipi kama ukimchukua huyo? Huyu hapa mmoja *hapa*, na mmoja *hapa*, na mmoja *hapa*, na mmoja, kila mahali tu. Mnaona? Na ni jambo la kusikitisha.

16 Ndipo unarudi, na kuwazia ya kwamba tunatupa kwenye pipa la takataka vya kutosha kuwalisha watu hao.

17 Na kuna kitu tu, uchumi wa ulimwengu haujasawazishwa mahali fulani, si sawa kabisa. Nasi hatuwezi kufanya lolote kulihusu, mnaweza kuona, lakini, mnaona, mimi ni Mmarekani mmoja tu. Na hiyo ni. . .na Mkristo mmoja tu. Nasi tunaweza kurudi na kusimulia hizo hadithi.

18 Na ni kweli kwamba wamishenari wengi, usiku wa leo, wanakula mlo mmoja ama miwili kwa juma, na bila viatu miguuni, suruali moja tu iliyochakaa, ama chochote kile, walichojifunika nacho, wakiingia misituni wakihubiri Injili, Injili hii tunayohubiri papa hapa. Kamwe si sawa kabisa, haionekani sawa, ingawa hawalalamiki, wanaendelea moja kwa moja kufanya hivyo, kwa vyovyote vile. Karibu tu inavunja moyo wako kuona.

Ninasema, "Jamaa yule *pale*?"

"Yeye ni mmishenari."

19 Tulipokuwa Durban, Afrika Kusini, huko ndiko nilikokuwa, nadhani, na wito mkubwa zaidi wa madhabahuni aliowahi kunipa Bwana, tulifikisha waongofu elfu thelathini kwa

wito mmoja wa madhabahuni. Wazia tu jambo hilo. Wenyeji elfu thelathini waliovaa mablanketi walimpokea Kristo kama Mwokozi wao walipoona yakitukia, kama tu vile mlivyoyaona hapa jana usiku. Wanaona njaa na kiu. Nao wanapoona jambo fulani ambalo lina uhalisi kwake! Bali angalieni, sisi hapa Marekani, tuna wainjilisti tu wa kila namna, na kama mmoja hatupendezi, tunamwacha tu, tunamchukua mwingine. Nanyi mwajua, tuna wa aina nyingi sana, na—na muda si muda mwajua, mbona, yote yanakuwa ni ya kawaida sana kwetu hata tunayasahau tu. Watu hao kweli wanamtamani sana Mungu.

20 Niliwaona wavulana wadogo weusi wamesimama namna *hiyo*, watoto wadogo, kamwe hawakujua suti ya nguo ni nini. Kamwe hawakujua . . . Vema, tulikuwa na aiskrimu ya kujitengenezea, ndipo mmoja wao angekuja, nami nikaiweka mkononi mwake, akaitupa na kupiga mayowe. Nikamwuliza Bw. . . . , ama, yule mtu aliyekuwa amesimama pamoja nami, "Alisema nini?"

"Alisema, 'Bosi, ilinichoma.'" Ilikuwa baridi, mnaona, kamwe hakuwa amehisi chochote baridi, mnaona. Akasema, "Ilinichoma."

21 Waangalieni kule chini, wanapoenda kuchota maji yao, nao mamba wanawatafuna. Kisha muwaone wakija angalau miezi miwili hivi kabla ya wakati, waliposikia nilikuwa nikija huko kuwaombea wagonjwa wao. Wangeenda wakiwabeba wapendwa wao kwenye machela ya kujitengenezea, mbao, na chochote walichoweza kuwa nacho. Nao wakati wangefanya hivyo, simba angekuja, wangewapandisha juu ya mti upesi mahali fulani mpaka hao simba waondoke, kisha wawashushe chini. Kujitolea kwa namna hiyo, huko chini kupitia misituni! Na kisha kuwaona wameketi angalau urefu wa bloku nne ama tano za mji, mpaka hata huwezi kuona mwisho wao namna hiyo, wameketi pale, ninii tu . . .

22 Ndipo walipomwona mtu mmoja ameponywa jukwaani . . . Nikageuka, na kupitia wakalimani kumi na watano mbalimbali, ni, inakubidi tu kuandika yale uliyosema mwisho, lakini nilipowauliza, je, mmishenari alikuwa amewaambia huyu Yesu mashuhuri alikuwa ni nani?

"Naam," lakini pia alikuwa amewaambia ya kwamba siku za miujiza zilikuwa zimepita.

Nikasema, "Sasa, Yeye alikuwa nini basi? Chochote alichokuwa wakati huo, anabaki yeye yule iwapo Yeye yu hai." Mnaona?

23 Basi walipoona hilo limethibitisha kwamba Yeye alikuwako, nilifanya tu maombi, maombi ya kusanyiko, ndipo Dk. F. F. Bosworth (Kuna mtu aliyewahi kusikia habari zake? Karibu kila mtu. Mmoja wa maskini watakatifu waadilifu sana niliopata kukutana nao maishani mwangu.), alikadiria kati ya miujiza elfu

ishirini na tano hadi elfu thelathini ilifanyika moja kwa moja kwa wakati mmoja.

Kesho yake asubuhi, Bw. Sidney Smith, meya wa—wa—wa Durban alinipigia simu, kasema, "Chungulia dirishani kuelekea ufukoni mwa bahari kutoka chumba chako cha hotelini."

Nikasema, "Ni kitu gani?"

Kasema, "Nitaona kama ninaweza kufika huko kwa wakati unaofaa, inakuja."

Vema, nilikuwa nimeketi pale, nikashangaa, "Meya alimaanisha nini?"

24 Na usiku huo tu, kulikuwa na mwanamke aliyekuwa amekufa kule siku hiyo, rafiki yake, nikamwombea, naye alikuwa amefufuka, magazeti yakiandika vichwa vya habari juu yake. Ndipo nikapanda juu . . .

25 Mnaona, watu kweli wanapojinyenyekeza, na kusahau mengine yote, na kumwamini tu Bwana, kila kitu kinatendeka tu. Ndipo basi . . . Lakini huna budi kuamini, hivyo tu, ninii tu, si—si kung'ang'ania tu kwake, bali rahisi tu, liamini, mnaona, ninii tu, kweli.

Na kwa hiyo, wakapiga simu. Ndipo nikasikia kitu fulani kikipiga kelele, nami nikashuka kwenda barabarani.

26 Sasa, wana—wana vita vya kikabila miongoni mwao, lakini nilipoenda jukwaani kulikuwako na makabila kumi na matano mbalimbali, najua, kule, wote mle ndani pamoja na wachawi wao, na machifu, na kadhalika, nao wote wamesimama kwa nia moja, karibu takriban laki mbili, na kuimba, kila mmoja katika lugha yao ya kienyeji, zote zikiungana pamoja, "Mambo yote yanawezekana, amini tu."

27 Ndugu Bosworth alisema alikuwa na wanamuziki wa simfoni waliofunzwa, naye akaenda Madison Square Garden pamoja na bendi yenye vifaa mia moja na kitu, naye akasema kamwe . . . kasema baadhi yao wangekuwa na sauti moja juu na sauti nyingine chini, kuzoeza sauti, lakini kasema kulikuwa—kulikuwa tu na kila mmoja, na hao, wasingejua mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, muziki mkamilifu kweli. Ninaweza tu kumwona wakati akitoa miwani yake, na kuanza kupangusa macho yake, akasema, "Ndugu Branham, huku ndiko kutawazwa kwangu, kuusikia huo."

Nikasema, "Huyo ni Roho Mtakatifu, Ndiye Kitu pekee ambacho kingeweza kuwafanya waimbe."

28 Kesho yake, nilipoenda dirishani na kuangalia nje, nilifikiri moyo wangu ungeruka unitoke, nikaangalia, yakishuka kuja barabarani yalikuwa malori saba makubwa ya Kiafrika. Yana urefu wa kama tu kutoka hapa hadi kwenye, loo, karibu jengo hili lote, yana magurudumu manne hadi sita chini yao. Nayo yalikuwa yamelundikwa juu kadiri yalivyoweza kulundikwa na

mbao kuukuu, na marungu, na vitu ambavyo hao watu walikuwa wametembelea siku iliyotangulia.

29 Na wale waliokuwa wakiyatumia walikuwa wakitembea nyuma, umbali wa majengo kadhaa ya mji. Sita kati ya hayo ma-. . .saba kati ya hayo malori makubwa yaliyojaa, namna hiyo, wakishuka barabarani huku wameinua mikono yao hewani, walikuwa viwete siku moja kabla wakiimba, "Mambo yote yanawezekana, amini tu." Nawaambia! Mnaona ni kwa nini . . . kile ninachomaanisha. Ni ninii tu, ni, moyo wako unatokwa na damu tu upate kuwafikia tena, unaona, unaruka tu kuona kile ungeweza kuwafanyia.

30 Nami nikachukua gazeti, moja ya gazeti la Durban, lililosema ya kwamba kabila moja, Washangaani, ninasahau ni kiasi gani walichorudisha majuma kadhaa baadaye, nao walikuwa, nao waliporudi, walikuwa wamemalizana na dhambi, wakarudisha bunduki, na saa, na yale waliyokuwa wameiba kwa kuishi kwenye hayo maboma, mwajua, wangeingia mjini, waibe.

31 Sasa samahani, dada zangu, kwa usemi huu fidhuli, wala msifikiri kwamba ninajaribu kufanya kitu fulani, kukishindilia. Lakini ninataka tu, kuwaulizeni tu jambo moja. Tunadhaniwa kuishi katika n—nchi ya ustaarabu. Na ubatizo huu wa Roho Mtakatifu tunaozungumzia, nimeona watu wakimpokea Roho Mtakatifu ambao hawakujua mkono wa kulia na wa kushoto. Nanyi mnajua wanachofanya wanapompokea? Wanatenda kama tu mnavyotenda mnapompokea, wanafanya jambo lile lile. Nao hawajui mkono wa kulia na wa kushoto ni upi. Nao wanawake walikuwa wamesimama kwenye uwanja huo pale, kama tu vile, hawana nguo, si zaidi ya zile walizozaliwa nazo, nao hao hapo wamesimama pale, vijana kwa wazee, na wote sawa.

32 Ndipo nikawauliza, nikasema, "Sasa, ninawatakeni . . . Je, mnaweza kumpokea huyu Yesu, ambaye amemfanya mtu huyu aliyekuwa kiwete kabisa kusimama wima na kutembea, ambapo alimwambia . . .?" Nami nikasema, "Mimi . . . Kwa vile wachawi wenu walidhani nilikuwa nikisoma mawazo yake." Nikasema, "Sasa, inaonyesha Mungu wa Mbinguni amemponya." Nikasema, "Ni wangapi wanaotaka kumpokea kama Mwokozi binafsi?" Nao wakasimama, maelfu.

Ndugu Baxter na hao wengine wakasema, "Ninaamini hapana shaka walimaanisha uponyaji wa kimwili."

33 Nikasema, "Lipitisheni kwa wakalimani tena." Nikasema, "Sikumaanisha uponyaji wa kimwili, nilimaanisha kumpokea Kristo, Mtu fulani anayekupenda. Nami ninatambua ya kwamba mlitendewa mabaya hapa, kama tu vile Mhindi wetu wa Marekani alivyotendewa kule, ambapo Mungu alimweka katika hiyo nchi." Lakini nikasema, "M—mlitendewa mabaya kwake, lakini kuna Mmoja atakayewapa haki, huyo ni Bwana Yesu, nawe ukitaka kumpokea kama Mwokozi wako binafsi, unaweza

kwenda Nyumbani Mbinguni." Ndipo nikasema, "Inueni mikono yenu. Hao waliobeba sanamu, zivunjilieni mbali ardhini."

Nao wakavunja sanamu zao, na kuinua mikono yao, makafiri elfu thelathini wanaovaa blanketi.

Nikasema, "Huku mmeinua mikono yenu, mpokeeni Yesu kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu."

34 Nao walipofanya hivyo, hao watu, wanawake fulani wamesimama pale, uchi, kijitambaa tu, mnajua walilofanya wapate kuondoka hapo? Walikunja mikono yao wapate kuondoka.

35 Sasa, ajabu kwangu ni kwamba, mwanamke asiyejua mkono wa kulia na wa kushoto, na mara Kristo anapokuja moyoni mwake, anatambua yu uchi, naye atajaribu kujificha, nasi, tunaodhaniwa kuwa ni taifa la Kikristo, tunaendelea kuzivua. Mwaweza kunielezea hilo? Ni—ninataka tu kuuliza swali hilo. Mimi . . . katika yote . . . Simaanishi hilo kufanya mzaha, hapa si mahali pa kufanyia mzaha, hili ni dawati, mimbara ya Mungu, mnaona. Lakini hiyo si ni kweli? Ni . . . Je, mnaweza kulielewa?

36 Mwenyeji asiyejua chochote kumhusu Mungu, na mara Kristo anapokuja moyoni mwao, wanatambua kwamba wako uchi, na sisi ambao tunadhaniwa kuwa Wakristo, daima kila mwaka, kadiri sheria itakavyowakinga msiondolewe mtaani, mnazivua kila mwaka. Kuna kasoro, mahali fulani. Labda ni . . . huenda ikawa ni mimi, huenda ikawa mimi ndimi tu nimekosea, sijui. Kama nimekosea, basi Neno limekosea, mnaona. Ninapenda kudumu na Neno.

37 Sasa, samahani, Billy, nilifanya hivyo tena. Ninaamini nilimwomba Ndugu Borders kusoma baadhi ya . . . Nina matangazo machache hapa, lakini nitayachukua tu baadaye kidogo, maana muda umeenda sana. Nami nitajaribu kuondoka saa tatu, nikiweza.

38 Sasa, ninataka kuchukua kutoka kwenye somo hilo la Maandiko kutoka katika Mwanzo, mlango wa 22, na *vifungu* kumi vya mwisho vya kifungu cha 17:

*na uzao wako utamiliki mlango wa adui zake;*

39 Sasa, tumekuwa tukijifunza juu ya Ibrahimu, na jinsi ambavyo Mungu alikuwa pamoja na Ibrahimu, na yale aliyomfanyia. Na Jumamosi iliyopita usiku, tulimwacha Ibrahimu, mwajua, ambapo Mungu alikuwa amemrudisha yeye na Sara kuwa kijana mwanamume na kijana mwanamke. Mlipenda hilo? Mnaliamini? Akarudi, naye akamzaa mtoto. Nasi tumethibitisha hilo kwa Maandiko ya kwamba Sara alikuwa msichana, kwa sababu kulikuwako na mfalme kijana kule chini, Abimeleki, aliyempenda.

40 Nami nilipata muhtasari kidogo juu yake, kasema, "Ndugu Branham, waliishi muda mrefu zaidi katika siku hiyo." Mtu

fulani kidogo alilipinga, bila shaka, hilo ni sawa tu, bali ningetaka kukufafanulia hilo, ndugu yangu.

41 Hivi uliona Maandiko yanasema, “Na wote wawili walikuwa na umri mkubwa”? Unaona? Walikuwa wazee. Na kwa hiyo aliwageuza wakawa kijana mwanamume na kijana mwanamke, akionyesha yale atakayoufanyia Uzao wote wa Ibrahimu. Sasa, tunaona ahadi hizo kuu alizotoa.

42 Ndipo tunaona ya kwamba Ibrahimu alikuwa mgumba; Sara alikuwa, labda, alikuwa tasa, labda Sara ndiye aliyekuwa tasa. Lakini baada, Ibrahimu, kwa kuwa mwili wake mwenyewe, kama Biblia ilivyosema katika Warumi 4, ulikuwa kama uliokufa, nasi tunaona ya kwamba hata hivyo miaka arobaini baadaye, mke wake alipokufa naye akaoa tena, alikuwa na wana wengine saba, mbali na binti, baada ya hapo. Kwa hiyo, mnaona, ni ninii tu, ninyi, katikati ya mstari, mnaona, Mungu aliwafanyia jambo fulani, hiyo ni kweli, Yeye aliwageuza tu, na kuwafanya mume na mke vijana tena.

43 Nina furaha sana kwamba nina nafasi, na ninaweza kuwaletea watu walioko ulimwenguni mojawapo wa hazina kuu sana, kuwaambia ya kwamba sisi ni warithi pamoja na Ibrahimu wa ahadi hii, sisi ni watoto wa Ibrahimu. Tunafanyaje hilo? Kwa kujiunga na kanisa? La. Kwa kuwa wafu katika Kristo, kumpokea Roho Mtakatifu. Basi sisi ni Uzao wa Ibrahimu, na ni warithi pamoja naye sawasawa na ile ahadi. Usikose kulipata, rafiki Mkristo, dumu nalo.

44 Kama kidogo nikifanya kama kupiga mbinja wakati nikizungumza, ninyi nyote mnajua ya kwamba nilikuwa bondia, nilikuwa nikipiga ndondi, nilishinda mashindano matatu ya taifa, sikuwahi kushindwa ila pigano moja maishani mwangu. Nami nilitabasamu kwa jamaa fulani wakati mmoja hapo alipo—aliponirushia ngumi na kunikosa, ndipo akanipiga moja kwa moja mdomoni, nayo ikalegeza meno mawili mle, na kuvunja kona ya moja. Halafu hivi majuzi tu, nilipoteza kile kijazo chake, kwa hiyo ni—ninapiga mbinja kidogo wakati mwingine.

45 Nilikuwa nikiwazia wakati mmoja jinsi jambo hilo lilivyokuwa baya, nami ninamkumbuka Bibi Graham, kwa ajili ya yule mwinjilisti mashuhuri, Billy, alisema ya kwamba ninii, moja ya nyakati muhimu sana za maisha yake ambapo, ameng’olewa jino moja la mbele, mwajua, naye anavaa la bandia, naye alipoteza jino hili, na ilikuwa karibu sana na wakati wake wa kuanza matangazo, basi akasema, “Anapiga mbinja vibaya sana, naye ananinii tu, na ilimbidi kusimama karibu na maikrofoni,” tena kasema, “loo, Billy kweli alikuwa akiomba.”

46 Ndipo bawabu, huku kila mtu akitafuta, hao wahudumu wakijaribu kutafuta jino hili, mahali lilipokuwa. Wakaja kugundua, lilianguka kutoka kwenye mfuko wa suruali

yake nalo lilikuwa kwenye kiatu chake, mtu fulani alilipata limeangukia kwenye kimoja cha viatu vyake. Ndipo—ndipo mkewe akalitaja kumhusu alipokuwa Louisville. Na kwa hiyo, jambo alilofanya, angechukua taulo baada ya kuoga, na kuitupa juu ya mlango namna *hiyo*, na kusababisha mchirizi mkubwa mchafu. Naye mkewe alikuwa mfupi sana asingeweza kusimama na kuupangusa, mwajua. Kwa hiyo, sote tuna makosa yetu, mnaona, sisi sote, hata kwa walio bora kuliko wote.

47 Kwa hiyo tunaona ya kwamba Ibrahimu na Sara sasa walikuwa wamempokea huyu mtoto. Katika umri wa yapata miaka kumi na miwili, alichukuliwa, akaulizwa na Mungu, ama, akampandishe mtoto wake mwenyewe mlimani na kumtoa kafara, kuutoa uhai wake.

48 Naye Ibrahimu hakukosa kumwamini Mungu, kwa sababu alijua ya kwamba kama yeye—kwamba kama angemtii Mungu kama alivyokuwa amemtii, alipongojea kwa muda wa miaka ishirini na mitano, kwamba alimpokea kama mtu *aliyetoka* kwa wafu (Sasa vipi kuhusu hilo? Walikuwa wazee au la?), kumpokea kama mtu aliyetoka kwa wafu, alijua ya kwamba alikuwa ameshawishika kabisa ya kwamba aliweza kumfufua tena kutoka kwa wafu. Mnaona? Kwa sababu alikuwa kama tu amekwisha kufa, uhai wake ndani yake, kama mwanamume, ulikuwa umekufa, naye Sara, tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa, naye alikuwa tu . . . Alikuwa tu amempokea kama mtu kutoka kwa wafu, kwa hiyo alijua ya kwamba Mungu angeweza kumfufua kama Yeye alitimiza ahadi Yake.

49 Ndipo tunaona wakati utii mkamilifu ulipokuja, basi wakati alipokuwa karibu kuutoa uhai wa mwanawe mwenyewe, Malaika wa Bwana aliita kutoka angani, na kuushika mkono wake, na kulikuwa na kondoo dume nyuma yake. Naye akamchukua kondoo dume aliyekuwa amenaswa kwenye magugu kwa ninii yake, ama, vichakani kwa pembe zake, na akamtoa huyo kondoo dume badala ya mwanawe mwenyewe. Nasi tulizungumzia hilo. Huyu kondoo dume alitoka wapi?

50 Sasa, Ibrahimu alikuwa kwenye safari ya siku tatu, ndipo basi akainua macho yake mbali sana na kuuona ule mlima. Alikuwa angalau maili sabini na tano hadi mia moja kutoka kwenye ustaarabu, na juu kwenye kilele cha mlima ambapo hakuna nyasi wala maji, naye alikuwa ameyafingirisha mawe kote, na kutengeneza madhabahu, wala hapakuwapo na kondoo dume pale. Na kama kondoo dume angekuwa huko juu, wanyama wangemwua muda mrefu uliopita, akipotea namna hiyo. Na hiyo ndiyo sababu alipaita *Yehova-yire*, “Bwana atajitolea Mwenyewe dhabihu.”

51 Ninaamini Mungu alimnena huyo kondoo dume akawepo. Nasi tuliona ya kwamba halikuwa ni ono, ono halitokwi na damu, alimchinja huyo kondoo dume, nayo damu ikatiririka

kutoka kwa huyo kondoo dume, ndipo akamtoa huyo badala ya mwanawe mwenyewe. Mnajua huyo kondoo dume alikuwa ni nani? Bwana Yesu Kristo. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ilikuwa, katika kunena kwa mfano, huyo alikuwa ni Yeye.

52 Ndipo Mungu akafurahishwa sana na utii mkamilifu! Mungu alikuwa amemjaribu mzee Wake, alikuwa amemjaribu mtumishi Wake. Na kila mwana amjiaye Mungu hana budi kufanyiwa kitu gani? Kujaribiwa, kurudiwa. Hapo ndipo ambapo wengi huangukia, kwa sababu hatuwezi kustahimili jaribio hilo.

53 Mtu anakuja madhabahuni wakati wa uamsho, nanyi mtaangalia kwa muda kidogo tu, wakati majaribu motomoto yanapoanza kuja, Yesu alifundisha hilo dhahiri, kasema, "Mpanzi alitoka akaenda akipanda mbegu, zingine zikaanguka kando ya njia, zingine zikaanguka penye mwamba, na penye miiba na michongoma, na zingine zikaanguka kwenye udongo mzuri."

54 Naye alisema hivyo ndivyo Neno lilivyoenenda, linavyotoka: Wengine husikia Neno, wanatoka nje, ndege wanakuja, wanalichukua, mnaona, hali—haliwafai kitu hata kidogo. Wengine wanakuja mara moja, loo, watafanya mambo makuu, lakini wakati majaribu yanapoanza kuja, yanawasonga kabisa. Lakini zingine zinaenda kote kwenye udongo mzuri, na hizo huzaa mara mia moja.

55 Hebu na tuwe ndio mara mia, hebu twende huko mbali, tuuze kila kitu kutoka ulimwenguni, na kumtazamia Kristo, na kumwamini Yeye kwa mioyo yetu yote. Hivyo ndivyo mambo haya yanavyotokea, hivyo ndivyo maono yanavyotokea, hivyo ndivyo nguvu kwa Mungu. . .za Mungu zinavyotenda kazi miongoni mwetu ni wakati sisi, hakuna shina la uchungu, na kila kitu kimesafishwa, na Roho Mtakatifu anaweza kutenda kazi kupitia kwetu, ndipo tunakuwa mfereji.

56 Vipi kama kulikuwa na shoti katika spika hii, usiku wa leo? Kamwe msingeweza kunisikia, yote ingekuwa na sauti inayokatikakatika, msingejua nilichokuwa nikisema. Vema, hivyo ni kama tu tulivyo sisi. Hicho ni—hicho ni bubu, mpaka kitu fulani kitoe sauti ndani yake, hakiwezi kuzungumza chenyewe. Na hivyo ndivyo tulivyo, hatujui lolote kuhusu mambo ya Mbinguni, bali inahitaji Roho Mtakatifu kushuka, na kutumia macho yetu kwa maono, midomo yetu kwa maneno na unabii, na—na—na kunena maneno, na kuona mambo yakitukia.

57 "Ombeni mtakalo katika Jina Langu, nanyi mtatendewa." Mnaona? "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa. Amin nawaambia, ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia,

yatakuwa yako uliyosema." Marko Mtakatifu 11:22 na 23. Sasa, tunajua ya kwamba mambo hayo ni kweli.

58 Sasa, tunaona ya kwamba Ibrahimu kwanza alijaribiwa. Naye akiisha kuyastahimili majaribio . . .

59 Nayo Biblia inasema kwamba sisi ni nini kama hatuwezi kustahimili marudio ya Mungu? Basi tunakuwa watoto haramu, *wanaojiita* watoto, bali si watoto halisi wa Mungu. Watoto wa Mungu wanajua mahali hasa wanaposimama, wanajua mahali wameweka tumaini lao, imani yao, matumaini yao, hakuna kitu kitakachowatikisa kutoka kwake.

60 "Wote alionipa Baba watakuja," hiyo ni kweli, na sasa, "yeye anijiaye Mimi sitamtupa nje kamwe. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hayo hapo Maandiko. Mnaona? Yohana Mtakatifu 5:24.

61 Wanaamini jambo hilo, wamelikubali, kuna jambo fulani lililowapata, wanakuwa kiumbe kipya. Wao ni asili mpya, wao ni—wao ni kiumbe kipya, kiumbe kipya. Hapo, neno la Kiyunani linasema, "uumbaji mpya." Ni kiumbe kipya, umeumbwa upya kutoka kwa kile ulichokuwa, ukawa sura ya mwana wa Mungu, na binti wa Mungu. Ni ninii tu . . . ndio mwujiza mkubwa kuliko wote uliowahi kutokea, wakati mwenye dhambi anaweza kufanywa kuwa Mkristo.

62 Kwa mfano, huu hapa mti wa miiba ukikua, ni—ni uhai, mti huu wa miiba, nao una miiba kila mahali, na una jani linalooneka la kiajabu-ajabu juu yake. Sasa, unaona, inahitaji kitu fulani mbali na kazi yoyote ya kibinadamu kuubadilisha mti huo wa miiba, na kufanya miiba hiyo kuuacha, na kufunuka tu, na kuwa majani mazuri sana, laini, na kuzaa machungwa. Sasa, mnaona, ni kitu gani ingebidi kitukie? Ingekubidi kuhamisha huo uhai wa mchungwa uutie kwenye mti huo wa miiba, ndipo basi kweli ungezaa machungwa, kwa sababu uhai ulio ndani yake ni wa mchungwa. Bila shaka, usingeweza kufanya hivyo kwa kawaida, ha—hautazalishika hivyo.

63 Lakini hivyo ndivyo tulivyo. Kama vile, sisi—sisi sasa ni nga—ngano, punje ya ngano katika ghala la Mungu, wakati tulikuwa gugu, naye Mungu akatubadilisha kutoka kwa gugu tukawa punje ya ngano. Huyafanya matunda kuwa tofauti, kubadilisha nia yako mwenyewe, mawazo yako mwenyewe. Ndio mwujiza mkubwa kuliko wote uliowahi kutokea, wakati mwanamume ama mwanamke anapozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, ndipo anakuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

64 Sasa, tunaona basi ya kwamba Mungu alimwambia Ibrahimu, "Kwa sababu umefanya jambo hili," kisha akampa huyo mzee wetu jaribu hili kuu, akasema, "Uzao wako utamiliki

malango ya adui. . .ya adui zake." *Maadui*, liko katika wingi. "Watamiliki malango ya maadui."

65 Sasa, Uzao wake. Sasa, Yeye anazungumza juu ya nani, ule *Uzao*? Huo Uzao ni Kanisa. Tunaingiaje Kanisani? Si kwa kujiunga Nalo, bali kwa kuzaliwa ndani Yake. Mnaona, ni—ninaamini ya kwamba tuna shirika letu, madhehebu yetu, na mambo hayo ni sawa, lakini hilo halituweki Kanisani. Tungeweza kujiunga na kila moja la hayo, na bado tusiwe katika Kanisa. Huninii, *hujiungi* na Kanisa, *unazaliwa* Kanisani. Unakuwa familia ya Mungu.

66 Sasa, nimekuwa katika familia ya Branham kwa miaka hamsini na mmoja, nao kamwe hawakuniomba nijiunge na hiyo familia, kwa sababu nilikuwa Branham wakati wa kuzaliwa, nilizaliwa katika hiyo familia. Mi—mimi ni Branham kwa kuzaliwa, hivyo ndivyo unavyofanyika Mkristo, kwa kuzaliwa. Unapozaliwa mara ya pili unakuwa kiumbe kipya, kiumbe kipya katika Kristo Yesu, ndipo mambo yote ya kale yamepita, na mambo yote yamekuwa mapya tena. Ni ninii. . .Ajabu!

67 Ningependa kuliuliza kanisa jambo moja: Ni hazina gani kuu zaidi ungaliweza kupata duniani, usiku wa leo? Ni kitu gani ungeweza kupata ambacho ungebadilisha na tumaini hili? Mbona, kusingekuwako na kitu ambacho kingeigusa kwa njia yoyote, kwa ajili ya tumaini hili kuu.

68 Sasa, lakini kumbukeni, "Uzao wako utamiliki malango ya adui zake." Uzao utamiliki. Sasa, Yeye anazungumza sasa juu ya Uzao wa Ibrahimu. Nasi tunakuwaje Uzao wa Ibrahimu? Kwa kuwa wafu katika Kristo, Wagalatia 3. Sisi, tunapokuwa wafu katika Kristo, tunakuwa Uzao wa Ibrahimu. Mnaona? Tu—tumekufa kwa mambo ya ulimwengu, na kuanza kiumbe kipya katika Kristo Yesu, basi Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani ya Kristo yuko ndani yetu, na hilo linatufanya Uzao wa Ibrahimu, na linatupa imani ya Ibrahimu. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu. . .

69 Watu wanasema, "Loo, siwezi kuamini katika uponyaji wa Kiungu." Nilikuwa nikizungumza na mhudumu fulani, sina kitu dhidi ya huyo mtu, yeye ana haki ya mawazo yake, yeye ni Mmarekani kama tulivyo sisi, naye akasema, "Ndugu Branham, sijali kama ungeweza kufanya miujiza elfu kumi, ni, bado siamini katika uponyaji."

70 Nikasema, "Bila shaka huwezi, ha—haukuwa kwa ajili ya wasioamini, ulikuwa ni kwa ajili ya wale tu wanaoamini." Mnaona? Hiyo ni kweli. Si—si kwa ajili ya wasioamini, ilikusudiwa tu waaminio, hivyo tu. Huyu Roho Mtakatifu ni kwa wale waaminio, uponyaji wa Kiungu ni kwa ajili ya wale wanaoamini, si wasioamini, ni waaminio.

71 Sasa, mnajua wao. . .Yesu alikuja kwenye wakati ule waliokuwa wakihubiri dhidi yake, na kadhalika, bali aliendelea moja kwa moja kuponya haidhuru. Na haidhuru wanazungumza

kiasi gani kuhusu "Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu," watu wanaendelea moja kwa moja kumpokea haidhuru. Mnaona? Huenda wasiweze kulielezea, hawawezi kuelezea ni molekuli ngapi zilizoko kwenye inchi moja, ama ni maili ngapi kufika mwezini, bali wanajua walipokea kitu *Fulani*, nao wanakifurahia.

72 Na, huu si mzaha, bali ulisemwa katika Wafanyabiashara Wakristo hivi majuzi, kwenye mmoja wa hiyo mikutano. Kulikuwa na dada mweusi mkongwe, aliyetaka kushuhudia, kidogo akausema kwa njia ya Kikusini, akasema, "*Mimi* inataka kutoa ushuhuda wangu." Akasema, "*Mimi* siko kile ninachotaka kuwa, wala *mimi* siko kile ninachopaswa kuwa, lakini hata hivyo siiko jinsi nilivyokuwa."

73 Kwa hiyo, nafikiri hivyo ndivyo Kanisa huenda likaweza kulisema, usiku wa leo. Huenda tusiwe jinsi tunavyotaka kuwa, na huenda tusiwe jinsi tunavyotaka kuwa, lakini, na vile tunavyopaswa kuwa, bali tunajua jambo fulani limetukia, hatuko vile tulivyokuwa. Ninajua hilo, kwa sababu umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Kuna jambo lililotukia, nasi tunalijua, jambo fulani lilitukia maishani mwetu, linalotufanya Uzao wa Ibrahimu, kwa sababu tuko ndani ya Kristo.

74 Sasa, Uzao wake, sasa, Yesu alisema kuhusu Uzao, alisema hivi, kwamba "Ingekuwa ni afadhali jiwe la kusagia lifungiwe shingoni mwako, na kuzamishwa katika kilindi cha bahari kuliko hata kumkosesha Uzao wa Ibrahimu. Aliye mdogo kuliko wote wa hawa waniaminio Mimi, itakuwa ni . . . " Ndipo Mungu akamwambia Ibrahimu, "Yeyote akubarikiye, nitawabariki; na yeyote akulaaniye, ninawalaani."

75 Sasa, baadaye kidogo katika juma hili sasa, nitapata *Muhuri Wa Mungu Na Alama Ya Mnyama*, na kugawa siku mbili usiku juu ya hilo, ninawatakeni mwe na hakika mnalipata kama mkiweza. Unasikia chati nyingi sana na kadhalika, lakini angalia jinsi ilivyo rahisi wakati Biblia inapolitoa, jinsi tu ilivyo rahisi kuliona, na sasa, ubaya na uzuri wake.

76 Sasa, kama utaangalia, Yeye alisema ya kwamba angembariki ambaye Ibrahimu . . . aliyembariki Ibrahimu na Uzao wake angebarikiwa, Naye angemlaani kila aliyemlaani Ibrahimu. Sasa, hebu angalieni tu jambo hilo katika Wayahudi, mwone kilichotukia; angalieni jambo hilo miongoni mwa Wakristo, mwone kilichotukia, vivyo hivyo daima. Kwa hiyo, mnaona, atamiliki lango la adui.

77 Hebu turudi nyuma na tuwaone baadhi ya watu wa Uzao wa Ibrahimu chini ya agano la Kiyahudi, kisha tulishushe katika Mataifa, wakati tulipopandikizwa kutoka wakati wa Kiyahudi hadi wakati wa Mataifa, kuchukua watu kwa ajili ya Jina Lake.

78 Sasa, hebu na tuchukue baadhi ya watu waliokuwa Uzao wa Ibrahimu, tuone kama walimiliki lango la adui. Hebu na

tuchukue kwa mfano, sasa, hebu tuzungumze kidogo juu ya, wakati wana wa Israeli walipokuwa wamechukuliwa mateka huko chini Babeli. Ulikuja wakati, kwanza, ambapo ilibidi jaribio lije. Daima kuna majaribu, sikuzote kuna giza zaidi kabla ya mapambazuko katika—katika maumbile, nawe daima utakuwa na majaribu kabla hujapata ushindi; kama hakuna vita, basi hakuna ushindi.

79 Na sasa, wale wana wa Kiebrania kule chini walikuwa wameletwa mahali ambapo mfalme alikuwa amefanya a—azimio, kwamba mtu yeyote asiyeisujudia sanamu hii angetupwa katika moto wa tanuru, tanuru ya moto, hasa. Ndipo wakati wao . . . *Hao* waliokusudia moyoni mwao, ya kwamba hawatajitia unajisi, wataishi karibu na Mungu. Sasa, wale wana watatu wa Kiebrania, Shadraka, Meshaki, na Abednego, walikuwa ni Uzao wa Ibrahimu, walikuwa na ahadi ya Mungu ya kwamba Uzao wake ungemiliki malango ya adui.

80 Sasa, ningewazia wakati jaribio lilipotokea . . . Ni kitu gani cha kwanza mtoto wa Mungu alicho nacho kama kimbilio wakati jaribu linapokuja? Silaha iliyo kuu sana, iliyopata kuwekwa mikononi mwa wanadamu, maombi. Hata inabadilisha kila kitu, hata ilibadilisha nia ya Mungu wakati mmoja. Mungu alimwambia nabii Wake aende akamwambie mfalme ya kwamba atakufa. Ndipo mfalme akaelekeza uso wake ukutani, na kusema, "Bwana, nakuomba unifikirie, Nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu. Ninahitaji miaka kumi na mitano zaidi." Naye Mungu akayaokoa maisha yake miaka kumi na mitano zaidi. Maombi hubadilisha mambo.

81 Ndipo tunaona basi wakati hawa wana wa Kiebrania walipokuja kwenye mkutano wa maombi usiku huo, "Tutafanya nini?" Ilibidi kuwe na m—mkutano, na ilibidi uamuzi ufanywe. Hapana shaka waliomba usiku kucha, ndipo uamuzi ukafanywa kwa kauli moja, kwa sababu walikuwa wakiamua kwamba wasingeweza kumwacha Mungu katika wakati wa majaribu.

82 Hilo si lingekuwa zuri kwa kanisa lote sasa? Uamuzi unapofanywa, "Je, niyarudie mambo ya ulimwengu? Niende kama hao wengine waendavyo?" Uamuzi huo humjia kila Mkristo, unakuja kwako kila siku. Tutafanyaje hilo? Huna budi kufanya uamuzi wako.

83 Basi wakajiamulia kwamba, hata iweje, hawatamwacha Mungu, hiyo ni kweli, kwa sababu walikuwa na ahadi ya Mungu ya kwamba walikuwa ni Uzao wa Ibrahimu, nao walijua mahali pao, pia walijua mahali walipokuwa wamesimama. Ndipo wakamwambia mfalme . . .

Wakasema, "Sasa," wakasema, "tutawatupa katika tanuru hii ya moto msipomsujudia mungu huyu."

84 Naye akasema, "Mfalme, ishi milele. Mungu wetu anaweza kutuokoa na tanuru hiyo ya moto, Yeye anaweza kufanya

hivyo, lakini asipofanya hivyo, bado hatutaisujudia sanamu hiyo. Tumeamua, tumeshika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, nasi tutasimama waaminifu kwake." Loo jamani! Huo ndio Kanisa linaohitaji.

85 Sasa, lazima uchukue hatua iyo hiyo inapofikia uponyaji wa Kiungu. Inapofikia jambo lolote ambalo Mungu ameahidi, chukua hatua na usimame hapo, Mungu alitoa ahadi. Yeye anawajibika kwa ahadi Yake, maadamu wewe ni Uzao wa Ibrahimu, Yeye hana budi kujibu. Sasa, usiingize mashaka yoyote niani mwako, ondolea mbali hayo mashaka. Kaeni tu moja kwa moja msalabani sasa, mwangalieni moja kwa moja Yeye aliyetoa hiyo ahadi.

86 Sijawahi kumwona akishindwa bado, wala sijawahi kusoma kuhusu Yeye akishindwa, wala kamwe hutamwona, kwa sababu Yeye hawezi kushindwa, Yeye ni Mungu. Yeye alitoa ahadi, aliifanya huko nyuma kabisa katika Mwanzo, huo ndio mlango wa mbegu, "Na Uzao wako utamiliki mlango wa adui." Si *adui*, *maadui*, kila mmoja wao, wote.

87 Sasa, adui huyu alikuwa ni ile tanuru ya moto. Kwa hiyo, ningeweza kuwazia asubuhi hiyo . . . Hebu tuigize hili kidogo tu. Linaonekana zuri sana moyoni mwangu ninapoona . . . Mwajua, wakiisha kufanya uamuzi wao . . .

88 Ninaamini Mungu husikia, bali si lazima Mungu sikuzote ajibu maombi papo hapo. Mnaona? Mungu hujibu kwa wakati Wake Mwenyewe. Kama ulimwomba, na kumwamini, basi atajibu kwa wakati Wake Mwenyewe. Kwa hiyo, ninawazia Utukufuni kulikuwako, walipokuwa wakiomba, ninaweza kuwaona Malaika wamesimama kukizunguka kile kiti cha enzi ambapo Mungu alikuwa ameketi, wakisema, "Wako katika maombi, wako chini ya mapambano."

"Naam, lakini watakuwa waaminifu, nina imani nao. Wao ni Uzao wa mtumishi Wangu Ibrahimu, kwa hiyo watakuwa waaminifu."

Vema, kesho yake asubuhi, huenda mfalme alisema, "Je, mmeamua sasa kwamba mtamsujudia mungu wangu?"

Kasema, "La, hatutasujudu. Vema, tutaninii tu . . . "

89 Iliiwasha hasira yake ndani yake, akaitia moto hiyo tanuru mara saba kuliko ilivyowahi kutiwa moto. Ndipo akachukua watu wakubwa wenye nguvu, wakaanza kwenda mbele wakawatupe kwenye tanuru. Nao walipokaribia, ilionekana kana kwamba ile saa ya giza ilikuwa imefika.

90 Hivyo ndivyo inavyoonekana kwa Wakristo wakati mwingine wakati mtu fulani, yule msichana, wakati ameshawishiwa na mvulana ambapo kweli anampenda kuvuta sigara yake ya kwanza; wakati anapolazimika, labda, kunywa ki—kinywaji kwa mara yake ya kwanza, kunywa kileo kikali

chake cha kwanza kwenye karamu ya bosi anayemfanyia kazi; ama mwanamume aliye na mke na familia nyumbani, huku huyo mwanamke mzinzi anapojaribu kufanya mapenzi naye, una vizuizi hivyo langoni, bali kama utaninii tu, ionekane kana kwamba Mungu amekuacha, lakini endelea tu kutembea imara, mwangalie Yeye, endelea tu kusonga mbele.

91 Nao wakaenda moja kwa moja. Na, mwajua, sisi ndio tunashikwa na wasiwasi. Nawe je, unayekubali uponyaji wako usiku baada ya usiku? Vema, unawazia, "Loo," kesho, "Ni—ni—ningali ninakohoa. Mkono wangu ungali umelemaa." Hilo halina uhusiano wowote nalo. Wakati kwa kweli, kwa uaminifu, kutoka kwenye kilindi cha moyo wako umekubali hiyo kama kazi iliyomalizika ambayo Kristo alikufanyia, imekwisha, ni hayo tu. Naam, bwana. Dumu tu moja kwa moja nalo.

Sasa, waliendelea kutembea, ninaweza kuwazia Shadraka alimwangalia Meshaki, kasema, "Una hakika tumeomba vya kutosha?"

"Loo, naam."

92 Wakasonga mbele moja kwa moja, tanuru ikizidi kuwa na joto zaidi na zaidi, mpaka karibu ngozi inatoka kwenye uso wao. Hata Biblia ilisema ya kwamba watu waliowatupa mle ndani, joto kali la tanuru hilo liliwaua wale watu waliowatupa ndani. Ilionekana kana kwamba ilikuwa ndiyo saa yenye giza kuliko zote, walijongea moja kwa moja mpaka ukingoni mwa tanuru.

93 Lakini, mwajua, wakati mwingine Mungu huacha iwe hivyo kukujaribu. Kamwe huwezi. . .Ibrahimu hangalimiliki mlango wa adui mpaka alipojaribiwa kwanza. Nawe kamwe hutamiliki lango la adui mpaka upitie majaribuni. "Wengine kupitia majini, wengine kupitia kwenye gharika, wengine kupitia majaribu mazito, bali wote kupitia kwenye Damu." Mungu huwaongoza watoto wake. Unaona, huna budi kujaribiwa kwanza.

94 Loo, ndipo mwana haramu huanguka katika majaribu, bali mtoto wa kweli wa Mungu husimama mkweli. Anajua mahali mali yake ilipo, anajua mahali anaposimama, anajua kilichompata, anajua ya kwamba amepita kutoka mautini kuingia Uzimani, naye anajua ya kwamba Mungu hujibu maombi.

95 Sasa, tunawaona wakipanda juu, hatua hii moja tu waingie kwenye tanuru ya moto, ilionekana kana kwamba walikuwa wameshindwa kabisa.

Huenda ikawa chini. . .Nimeona wagonjwa wa kansa wakififikia karibu pumzi yao ya mwisho.

96 Ndugu mmoja aliyeugua yabisi kavu, hivi majuzi, alikuwa ameweka mikono yake namna *hii*. Roho Mtakatifu akamwambia, akasema, "BWANA ASEMA HIVI, umeponywa."

97 Alienda nyumbani na kuwa katika hali mbaya zaidi. Akasema, "Siwezi kujizuia, mtu huyo hakunijua, hajawahi kuniona maishani mwake." Aliishi Phoenix. Akasema, "Hajawahi kuniona maishani mwake. Angewezaje kuniambia nilikuwa nani? Ninajua kwa matamshi ya huyo mtu, yeye si mwalimu. Ninajua ya kwamba kulikuwa na *kitu fulani* cha kimbinguni. Nami. . .jambo fulani lilitukia."

Wasingeweza hata kusogeza mto, walipousogeza mto kwa ajili ya mikono yake, angesema, "Loo, mke wangu, mke wangu, kuwa mwangalifu!" Loo, akipiga tu mayowe.

Naye akasema, "Mpenzi, hivi huogopi unaleta aibu juu ya dini ile ile tunayoamini?"

Kasema, "Siwezi! Ninaamini hilo moyoni mwangu kwamba litatukia."

98 Ndipo hali ikawa mbaya sana, akalala, naye maskini msichana wake alikuwa akijaribu kuweka kitambaa kilicholowa maji usoni mwake, alijisikia kuzimia, ndipo akaangalia juu pale, naye akasema alimwona Kristo amekuja mbele yake msalabani. Naye akasema, alipoinamisha kichwa chake apate kufa, alifikiri pumzi yake ilikuwa ikienda, asingeweza kupumua tena, alijaa yabisi kavu, ndipo wakati alipoinamisha kichwa chake afe, alimwona Kristo akiinamisha kichwa Chake pale, kwa ghafla akafanya mruko mkubwa, naye huyo akatoka kitini, na kuzunguka na kuzunguka na kuzunguka mahali hapo.

Na hilo, kwa nini? Yeye alimiliki lango alipopitia kwenye hilo jaribu. Lakini kwanza, huna budi kumiliki. . .lazima upitie jaribuni.

99 Wale wana wa Kiebrania walikuwa mahali hapo. Wakati mwingine tunafikiri ni giza sana, lakini kumbukeni, ni katika saa yenye giza kuliko zote ndipo Yesu ajapo.

100 Ilikuwa ni Mariamu na Martha, maskini dada zake Lazaro, Familia ya Kikristo ilikuwa imeondoka kwenye sinagogi lao ili kumwamini Bwana Yesu, na ilikuwa ndiyo saa yao yenye giza kuliko zote.

101 Walitoka kanisani mwao, wasingeweza kurudi tena, yeyote aliyekiri kuwa mfuasi wa Yesu alifukuzwa kanisani kwa sababu Yeye alikuwa m—mlokole, Mtu fulani akizunguka-zunguka na kuyararua makanisa yao. Nao hawakutaka jambo hilo, kwa hiyo wakasema, "Mtu yeyote anayejaribu kumfuata, mbona, tutawatupa nje ya ushirika." Kwa hiyo walikuwa nje ya ushirika. Nao wasingeweza kurudi kanisani, walikuwa wazushi.

102 Halafu basi, Mtu yule yule waliyetoka kwa ajili yake, Bwana Yesu, Mtu yule yule waliyemtokea, walituma mtu Kwake aje akamwombee ndugu yao alipokuwa amelala, akifa kwa kutokwa na damu, nao. . .Yeye alikataa kuja. Wakatuma mtu mara ya pili, Naye akakataa kuja. Loo, jinsi saa hiyo ilivyokuwa na

giza wakati huo! Hatimaye, saa ya usiku wa manane ikafika, ikawadia, ndipo mvulana huyo akafa. Wakamweka kaburini, alikuwa humo siku nne, uharibifu tayari ulikuwa umeingia mwilini mwake. Mabuu ya ngozi yalikuwa ndani yake, wadudu kutoka ardhini walikuwa wakitambaa kuingia mwilini mwake, saa yenye giza kuliko zote waliyopata kuona, wakati huo ndio Yesu alipopitia, kwenye saa hiyo tu yenye giza.

103 Loo, mwanamke ambaye, alisema si muda mrefu uliopita, alisema, "Ndugu Branham," nilikuwa nikizungumza kuhusu kumfufua Lazaro, kasema, "Humaanishi kuninii. . . Unajivuna sana kuhusu Yesu kuwa ni Mungu."

Nikasema, "Yeye alikuwa ni Mungu, naam."

Akasema, "Vema, nitakuthibitishia kwa Biblia yako kwamba hakuwa."

Nikasema, "Iendee."

Naye akasema, "Vema, mlango wa 11 wa Yohana Mtakatifu ulisema alienda kwenye kaburi la Lazaro, akalia."

104 Nikasema, "Hilo—hilo halikuwa na uhusiano wowote nalo, Yeye alikuwa mwanadamu na Mungu pia." Nikasema, "Yeye alikuwa mwanadamu, kweli, alipokuwa akilia, lakini aliposimama kando ya kaburi la mtu aliyekuwa amekufa siku nne, na pua yake tayari imebonyea ndani, wadudu wakila mwilini mwake, kasema 'Lazaro, njoo huku,' hiyo ilihitaji zaidi ya mwanadamu." Naam, bwana.

105 Alikuwa mwanadamu wakati aliposhuka kutoka mlimani usiku ule, wakitafuta kitu cha kula kwenye huo mzeituni, wala hawakupata kitu pale, Yeye alikuwa mwanadamu alipokuwa na njaa, lakini alipochukua biskuti tano na vipande viwili vya samaki na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, naam, bwana, huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mtu huyo. Naam, bwana.

106 Alikuwa ni mwanadamu amelala huko nje nyuma ya meli hiyo ndogo usiku huo, pepo, arobaini elfu wao, wa baharini, waliapa wangemzamisha, maskini meli hiyo kama kizibo cha chupa huko nje, ikirushwa-rushwa, ibilisi akasema, "Tumempata sasa, amelala. Tutamzamisha." Yeye alikuwa ni mwanadamu, mchovu na amedhoofika, amelala nyuma ya mtumbwi ule pale, akiwa na mto mahali fulani, amelala usingizi. Lakini, ndugu, mara alipoinuka, loo jamani, aliweka mguu Wake kwenye demani ya chombo, akaangalia juu, na kusema, "Amani, tulia," na pepo na mawimbi yakamtii, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mwanadamu huyo.

107 Ilikuwa ni mwanadamu aliyelia apate rehema msalabani, hiyo ni kweli, "Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Alikufa akililia rehema, hiyo ni kweli. Lakini katika asubuhi hiyo ya

tatu, wakati alipovunja mihuri ya mauti, na kufufuka tena siku ya tatu, na kupaa Juu, Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu.

108 Kila mtu aliyepata kuwa kitu chochote aliamini hilo. Hiyo ni kweli. Washairi, waandishi, manabii, wowote wale, wanaamini hilo.

109 Sasa, wale wana wa Kiebrania, wakipitia majaribu yao, walikuwa moja kwa moja wamefikia dakika ya mwisho, walikuwa tayari tu kuingia kwenye ile tanuru. Mnajua nini? Wakati mwingine tunaangalia mambo yakiendelea hapa duniani, lakini kuna jambo fulani linaloendelea Mbinguni wakati uo huo. Huenda tusiweze kuliona, bali linaendelea, kwa vyovyote vile. [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] (Samahani.)

110 Hebu tugeuze kamera yetu sasa kuelekea Mbinguni. Ninaweza kumwona Yesu ameketi kwenye Kiti cha Enzi, kukipambazuka, moshi unapaa juu sana angani kutoka kwenye hiyo tanuru, ninamwona ameketi pale akiangalia chini, aone kile watakachofanya. Hivyo ndivyo anavyotufanyia mimi na wewe tunapojaribiwa. Yeye aliahidi ya kwamba Uzao wa Ibrahimu utamiliki lango la adui, ninaamini hilo.

111 Ninamwona akiangalia, mara, Malaika mkuu anakuja upande wake wa kuume, anasimama mguu sawa, anaweka mkono wake juu ya upanga wake, Gabrieli, kasema, "Baba, umeangalia kule chini? Wao ni Uzao wa Ibrahimu. Wao ni, wanakuamini Wewe, waliomba usiku kucha, nao wanaingia moja kwa moja kwenye mauti yao. Hebu nishuke niende kule, nitabadilisha hayo mandhari." Ninaamini angeweza kufanya hivyo. Hiyo ni kweli.

Akasema, "Hiyo ni kweli, Gabrieli. Wewe ni Malaika mzuri, simama tu hapo."

112 Huyu hapa mwingine anakuja, jina lake ni Pakanga, yeye ndiye Ma—Malaika anayetawala juu ya maji yote. Ninamwona amesimama mguu sawa, kasema, "Baba, umeangalia huko chini Babeli?"

"Naam, nimewaangalia usiku kucha." Loo, jicho Lake liko juu ya shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia. "Nimewaangalia usiku kucha."

113 "Wanajiandaa kuwateketeza watu watatu huko chini asubuhi ya leo, Wazao wa Ibrahimu ambao wameamini Neno Lako, na wanalitetea kishujaa. Unajua wakati mmoja uliniambia niyafungulie maji yote. Nina mamlaka, naomba nishuke kule, nitaifagilia mbali Babeli kutoka kwenye ramani." Angeweza kufanya hivyo.

114 Ninaweza kumsikia akisema, "Hiyo ni kweli, Pakanga, wewe ni Malaika mzuri sana. U—ulifanya kila kitu hasa nilichokwambia tangu ulipoumba. . .Nilipokuumba. Ulifanya

hivyo, pia, Gabrieli. Lakini mnajua, ninashuka Mwenyewe, hii ni kazi Yangu." Loo jamani!

115 Wakati tu walipokuwa tayari, kuchukua hatua yao ya mwisho, ninaweza kumwona akisimama, majoho Yake ya ukuhani yanamwangukia mahali anapoketi usiku wa leo. Yamelowa Damu, akituombea tunapokiri, kwa kuwa Yeye alikufa apate kutimiza lolote tuombalo. Iko wapi imani yetu katika Yeye?

116 Huyo hapo amesimama, akiashiria upande *huo*, na hili hapa wingu kubwa jeupe linakuja, anapanda juu yake, anaita upepo wa mashariki, upepo wa kaskazini, upepo wa kusini, na upepo wa magharibi, apate kuyapanda kama farasi, ananyosha mkono, anashika radi ya zigizaga, anairusha angani. Kabla hawajaweza kuingia mle, Yeye alikuwa ndani ya tanuru ya moto pamoja nao.

117 Akasimama mle ndani pamoja na pepeo kubwa la mtende pale mahali fulani la Mti wa Uzima, likiipepeta hiyo miali ya moto namna *hiyo*, Kasema, "Nilitaka tu kulizungumzia pamoja nanyi watoto. Ninajua ya kwamba ninyi ni Uzao wa Ibrahimu, nilitoa ahadi, nami nipo hapa kujibu, njoni hapa," akiizuia hiyo miali ya moto, loo, naam.

Wakaifungua, kasema, "Mliwaweka wangapi mle ndani?"

Kasema, "Watatu."

118 Akasema, "Kuna Mmoja zaidi mle ndani, Naye anaonekana kama Mwana wa Mungu." Alikuwa. Kwa nini? Wao, baada ya kujaribiwa, walimiliki lango la adui. Amina.

119 Danieli aliletwa kwenye jambo lile lile baada ya kujaribiwa kama angeomba au la. Akainua mapazia nyuma, akatupa mashuka, kisha akapiga magoti na kuomba, kama tu alivyofanya daima. Naam, bwana. Akaomba kama tu alivyofanya sikuzote. Basi kukafanyika nini? Walipitia majaribuni.

Wakasema, "Tutakulisha kwa simba," nao walikuwa wamenyimwa chakula kwa majuma kadhaa.

Kasema, "Mungu wangu anaweza kuniokoa na hao simba."

Lakini akiisha kupitia kwenye hilo jaribu, kulifanyika nini? Alimiliki lango la adui. Kwa nini? Alikuwa mwaminifu kwa Mungu.

120 Musa, baada ya kuwa mwaminifu kwa Mungu, alipitia majaribuni, na kuwaleta wana wa Israeli moja kwa moja kwenye wajibu wao, maumbile yote yalipiga makelele dhidi yake, hii hapa milima upande mmoja na majangwa, jeshi la Farao likiwafuata, nayo Bahari ya Shamu ikawazuia. Mbona, walikuwa wamenaswa! Ilionekana kana kwamba Mungu alikuwa ni mwanajeshi duni, kuwasukumia mle pembeni moja kwa moja na kuwaacha waangamie.

121 Mungu anapenda kufanya hivyo. Mungu anapenda kuonyesha mkono Wake wenye nguvu. Naam, Yeye hufanya hivyo. Anapenda kuonyesha nguvu Zake. Anangojea usiku wa leo kuwaonyesha, kumchukua huyo mwenye dhambi na kumgeuza, kumchukua mwanamke huyo mwenye sifa mbaya na kumbadilisha awe mwanamke mtauwa, mtakatifu, kumchukua msichana huyo ambaye ameshika njia mbaya, mvulana huyo kwenye njia mbaya, kuwarudisha mahali fulani, na kuwafanya wana na binti za Mungu.

122 Yuko tayari kumchukua mtu huyo anayekufa kwa kansa, huyo aliye na ugonjwa wa moyo, huyo aliye kipofu, huyo anayeteseka, kama tu ataweka imani yake mle ndani apate kumgeuza atoke mautini aingie uzimani, amwanzishe na ushuhuda.

123 Yeye anangojea kufanya hivyo, anakuweka moja kwa moja mtegoni aone unalofanya. Aliwaweka moja kwa moja kwenye mtego huo pale, ilionekana kana kwamba maumbile yenyewe yalikuwa yakiuficha uso wake. Naam.

Mwandishi mmoja alisema wakati mmoja, ya kwamba walipofika mahali hapo, walishangaa yale Musa angefanya. Walikuwa na amri moja, “Nendeni mbele.”

124 Kama uko kwenye wajibu, haidhuru ni kitu gani kinachokaa njiani, tukio kuu sana nililowahi kuwa nalo ni kukabiliana na kitu ambacho nisingeweza kupita juu yake, ama chini yake, kusimama tu hapo na kumwona Mungu akitengeneza njia ya kupitia kwake. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo, songa tu, endelea kusonga mbele, sukuma kwa pua yako. Endelea tu kusonga mbele, endelea tu kusonga mbele, Mungu atafanya njia.

Yule mzee, mtu mweusi huko kusini aliyebeba Biblia, wao wakasema, “Kwa nini unabeba Biblia hiyo, Mose? Huwezi kusoma.”

Kasema, “Ninaiamini.”

Kasema, “Vema, u—unajuaje ni ya kweli?”

Akasema, “Vema, ni, ninaiamini kutoka *chalada* hadi *chalada*, *chalada* pia.” Anasema, “Imeandikwa Biblia Takatifu juu yake.”

Kasema, “Nadhani unaamini yote yaliyo humo ndani?”

Kasema, “Naam, bwana.”

“Nadhani unaamini lolote Mungu angekwambia ufanye, ungelifanya?”

Akasema, “Ningelifanya.”

Kasema, “Vipi kama Yeye angekwambia, ruka kupitia kwenye ukuta ule, ule ukuta wa mawe? Utapitiaje humo?”

125 Akasema, “Kama angeniambia niruke, ningeruka, Yeye angetoboa shimo nitakapofika pale.” Kwa hiyo hiyo ni kweli.

Kwa hiyo hilo ndilo jambo unalopaswa kufanya, ni kumchukua Mungu, na kuliamini, na kuruka, kwa vyovyote vile.

126 Kama unajua ungeweza kulielezea, kulielewa, basi haingekuwa ni imani tena. Imani yako ni yale unayoamini kwamba Yeye amekufanyia. "Nayo imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Hulioni, huwezi kulielewa. Hakuna njia ya kumwelewa Mungu, inakubidi tu kumwamini, na uendelee kutembea. Yeye alisema hivyo.

127 Hivyo ndivyo ninavyosimama mimbarani kwa ajili ya maono. Hilo ndilo . . . Yeye huniambia niende nikafanye mambo fulani ambayo yanaonekana kuwa hayawezekani kibinadamu, nanyi nyote mnajua hilo, haiwezekani kibinadamu, bali Yeye alisema ulifanye, endelea tu, Yeye Ndiye atakayelishughulikia, Naye atafanya hivyo. Naam. Jinsi Wewe ulivyo mkuu!

128 Wakati Musa aliponasiwa mahali hapa, sasa, yeye yuko moja kwa moja katika wajibu wake, moja kwa moja katika wajibu wake, Mungu alimwongoza moja kwa moja kule chini. Anaenda kufanya nini? Bahari ya Shamu, mtego uliotegwa vilivyo, lakini Musa aliendelea tu kusonga mbele.

129 Mwandishi mmoja, ninaamini, alisema ya kwamba Mungu aliangalia chini kupitia ile Nguzo ya Moto kwa macho yenye hasira, akaiangalia Bahari hiyo ya Shamu iliyokuwa ikijaribu kuwakatilia mbali watoto Wake wakiwa kwenye wajibu, naye akasema hiyo bahari iliogopa, na kurudi nyuma, na kuwatengenezea tu njia.

130 Vema, kama angeweza kuangalia kupitia Nguzo ya Moto na kufanya hivyo, ingekuwaje wakati alipomwangalia mwenye kukiri aliyesimama hapo kupitia Damu ya Mwanawe Mwenyewe, pamoja na ahadi ambayo Mungu aliapa ataishughulikia, na kuapa ya kwamba angeishughulikia, ya kwamba Uzao Wake wa Ibrahimu utamiliki malango ya adui? Hakika. Yeye anawajibika kufanya hivyo kwa Damu ya Mwanawe Mwenyewe iliyowekwa kwenye kiti cha rehema, usiku wa leo. Loo, laiti tungeweza kuachana na mawazo haya ya kidunia, na kuangalia huko juu, tuone ni Nani aliyetoa hiyo ahadi, Mungu Mwenyewe wa uumbaji! Naam.

131 Yoshua, pia, baada ya kupata jaribio huko Kadeshi, alirudi, asilimia tisini ya wahudumu walisema, "Hatuwezi kuichukua."

132 Yoshua akasema, "Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka," yeye na Kalebu. Naye alikuwa mmojawapo wa wale wawili pekee kati ya watu milioni mbili na nusu waliovuka. Alifanya nini? Alishuka akaja Yordani, ilikuwa ikimzuia asiingie kwenye nchi ya ahadi, bali alimiliki lango la adui. Kwa nini? Kwa sababu aliamini Neno la Mungu, alikuwa amejaribiwa, naye akaliamini, alijua Mungu alitimiza Neno Lake, kwa hiyo akamiliki lango la adui.

Ningeweza kuendelea na kuendelea, lakini nimepitisha wakati.

133 Mashujaa hawa wote wakuu, kila mmoja wao, walifanya mambo makuu, wao—wao...miujiza mikuu, na kuzunguka-zunguka huku wamevaa ngozi za kondoo, majangwani, nao walikuwa wahitaji, na wengine wakakatwa kwa misumeno, na mambo yote mbalimbali. Kama vile Waebrania 11 inavyosema, mashujaa hawa wote wakuu walishuka wapate kufa, kila mmoja wao alishuka apate kufa, lakini siku moja, siku moja tukufu, ule Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu akaja, aliyezaliwa na bikira. Naam.

134 Wakati alipotembea duniani, Yeye alikuwa Uzao wa kweli wa Ibrahimu. Alitembea duniani, akamiliki lango la magonjwa kwa ajili ya watu, akamiliki lango la mateso. Yote Yeye... Katika bustani ya Gethsemane, uani asubuhi hiyo, Yeye alimiliki malango ya majaribu. Juu ya Mlima wa Kugeuka Sura, hapo alijithibitisha Mwenyewe.

135 Wakati ibilisi alipompeleka kwenye mlima mwingine, alikuwa na nguvu juu ya adui kuonyesha ya kwamba angeweza kufanya hivyo. "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate."

136 Haikumbidi kufanya hivyo, Yeye alisema, "Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu." Alichukua Neno la Mungu maana Yeye alikuwa ni Uzao wa kweli wa Ibrahimu, kisha akamiliki kila baraka ambayo Mungu aliahidi. Naam, bwana.

137 Alisimama pale chini ya majaribu, kasema, "Ningeweza kuzungumza na Baba Yangu mara moja, Naye angenitumia Mimi majeshi ishirini ya Malaika." Mmoja angeweza kufanya nini? Majeshi ishirini ya Malaika, wangeweza kuibadilisha kama wangetaka. Hiyo ni kweli. Lakini ilibidi ajaribiwe kwa njia zote kama sisi. Akisimama pale huku makonzi ya ndevu yameng'olewa usoni Mwake, na ile Damu na dhihaka, mate ya walevi kutoka kwa askari yakining'inia usoni Mwake.

138 Waliweka kitambaa juu ya kichwa Chake namna *hii*, na kumpiga kichwani kwa mwanzi, kasema, "Sasa ulisema ulikuwa nabii, unaweza kusoma mawazo ya watu, twambie ni nani aliyekupiga. Tuambie ni nani aliyekupiga." Angeweza kufanya hivyo, bali angekuwa akimsikiliza ibilisi. Alimiliki lango la adui, alistahimili majaribu. Ee Mungu, tupe Mtu kama huyo! Hiyo ni kweli.

139 Ndipo wakati alipokufa pale msalabani, kuzimu kuliichukua Nafsi Yake ya thamani. Biblia ilisema Nafsi Yake ilishuka kuzimuni. Hiyo ni kweli kabisa. Kuzimu iliiteka Nafsi Yake, na kumpeleka kule chini. Lakini ndugu, katika siku hiyo ya tatu Yeye alimiliki malango ya mauti, kuzimu, na kaburi, akafufuka siku ya tatu, akashinda yote. Alichukua maradhi, mauti, kuzimu, kaburi, na kila kitu.

140 Ninaamini Yeye aling'oa hilo lango moja kwa moja kutoka kwenye bawaba zake, na kuwatoa nje, akapanda Juu, akapaa Juu. Na, usiku wa leo, ninyi ni zaidi ya washindi. Uzao Wake utamiliki malango ya adui. Naam, bwana. Alimiliki kila lango, alishinda kila ugonjwa, alishinda kila dhambi, alishinda kila jaribio, Alishinda mauti, akashinda kuzimu, akashinda kaburi, akamiliki lango la hayo yote. Nasi ndani Yake ni zaidi ya washindi, wakati tukiwa ndani Yake, maana Yeye alishinda kwa ajili yetu. Loo, laiti tungalijua huo Uzao wa kweli wa Ibrahimu ulikuwa ni nini, kile hasa ulichomaanisha kwetu!

141 Ibilisi alimtilia shaka. Ibilisi, huo ulikuwa ni wakati mmoja ambapo alifunikwa kwa sufu, kama tusemavyo, machoni mwake. Wakati alipompeleka juu ya mlima, kama nilivyokuwa nikizungumzia muda mfupi uliopita, alisema, "Hiyo inaweza kuwa? Mtu huyo ni nabii tu. Je, anaweza kuwa ndiye Mwana wa Mungu?" Akasema, "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu," ilionyesha alilitilia shaka, "ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yafanywe mkate, kwa sababu una njaa, umekuwa ukifunga siku arobaini, kula."

Yesu akasema, "Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate pekee."

142 Akampeleka juu ya kinara cha hekalu, kasema, "Jitupe chini, kwa maana imeandikwa, Yeye atawaagiza Malaika kwa ajili Yako, usije wakati wowote, ukajikwaa mguu Wako kwenye jiwe, watakuchukua."

Akasema, "Naam, na pia imeandikwa..." Kila kitu, Yeye alikabiliana naye kwa Neno la Mungu, kwa sababu Yeye alikuwa Uzao wa kweli wa Ibrahimu.

143 Alimiliki kila mlango wa majaribu. Loo, jinsi alivyofanya! Yeye alikuwa ni Mwanadamu, alikuwa Mwanadamu kama ulivyo wewe, kama nilivyo mimi. Alikuwa na haki ya kuoa, alikuwa na haki ya kuwa na boma, alikuwa na haki kwa mambo tuliyo nayo, alikuwa na haki ya kuwa na nguo. Angeweza kufanya hivyo, Mtu ambaye angeweza kugeuza maji kuwa divai, ambaye angeweza kujua mahali sarafu ilipokuwa katika kinywa cha samaki, mbona, Yeye alimiliki mbingu na nchi, bali hata hivyo alijiepusha na mambo hayo.

144 Maneno matamu kuliko yote katika Biblia aliposema, "Baba, najitakasa Mwenyewe nipate kuwatakasa." Alikuwa akijaribu kufanya nini? Kuweka mfano. Alikuwa akiwatuma watu kumi na wawili pamoja na Injili ambayo ingeushinda ulimwengu, Naye anatutegemea mimi na wewe kufanya hivyo. Kama angeweza kujitakasa Mwenyewe namna hiyo, mbona, inatupasa kuweka kando kila kushindwa, na kila shaka, na kila kitu kingine, na kujitakasa! Kwa kuwa sisi ni Uzao wa Ibrahimu kupitia Kwake, ambao ni zaidi ya washindi kupitia Yeye. Naam.

145 Alikuwa na haki ya kuoa, alikuwa na haki ya kuwa na boma, alikuwa na haki ya kuweka kichwa Chake juu ya mto, lakini “Mbweha wana matundu, na ndege wana viota; na Mwana wa Adamu kamwe hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake.” Kwa nini? “Ninajitakasa, Baba, kwa ajili yao, ninafanya hivyo.”

146 “Kwa ajili yao,” si kwa sababu ilimbidi kufanya hivyo, bali “kwa ajili yao,” Yeye alimshinda kila adui.

147 Akiwa amesimama pale kwenye chumba cha mahakamani siku hiyo, ama, uani, alipokuwa amefanyiwa mashtaka na kushtakiwa kwa uongo, jambo pekee walilopata dhidi Yake lilikuwa ni kuvunja siku ya Sabato, Yeye alisema, “Mimi ndimi Bwana wa Sabato,” na alikuwa Ndiye. “Akijifanya Mwenyewe Mungu,” Naye alikuwa ni Mungu. Na hapo, mashtaka hayo yote ya uongo na kadhalika, na mashahidi wa uongo waliokuwa washtaki Wake. Hatimaye, akapigwa kwa pigo kubwa mpaka mbavu Zake zikatokeza, nalo maskini joho dogo alilokuwa nalo mgongoni Mwake, walilivua, wakampiga kwenye nguzo. Ilikuwa ni kitu gani? Huyo alikuwa ndiye Uzao wa kweli wa Kifalme wa Ibrahimu.

Hapo ndipo tunaposimama, usiku wa leo:

> Imani yangu haijajengwa juu ya kitu chochote pungufu
> Ila Damu ya Yesu na haki;
> Wakati yote yanayoizunguka nafsi yangu yakitoweka,
> Basi Yeye ndiye Tumaini langu lote na Ngome.
>
> Kwa kuwa juu ya Kristo, Mwamba huo imara, ninasimama;
> Ardhi zingine zote ni mchanga udidimiao,
> Ardhi zingine zote ni mchanga udidimiao.

Hapo ndipo ninapopeleka tumaini langu, papo hapo kwenye huo Mwamba imara.

148 Enyi Uzao wa Ibrahimu, Yeye alimiliki kila lango, hata la mauti na kuzimu. Mwangalieni Yeye pale. Alikuwa na dhihaka . . . Mwanamke yule akijaribu kutawadha miguu Yake tena. Wakaweka kitambaa usoni Mwake, na kusema, “Kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga, tutakuamini.”

Msalabani walisema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka, nasi tutakuamini.”

Hawangemwamini kwa vyovyote vile, haijalishi alifanya nini; Yeye hakuwajali.

149 Hebu tumwangalie kidogo asubuhi ya leo, ama, usiku wa leo. Ilikuwa ni asubuhi mbaya sana asubuhi hiyo. Tumerudi chumbani. Hebu tuninii tu, nitalichukua kusanyiko hili, ninawatakeni mwangalie jambo fulani. Hebu twendeni dirishani, nasikia umati unaoomboleza. Kuna nini? Inua

pazia uangalie nje. Ninasikia kitu fulani kikigongagonga, kikishuka kuja barabarani. Ni kitu gani? Msalaba ukikokota, ukishuka mtaani, *kung'u-kung'u*, juu ya hayo mango ya kale, ukipanda kwenda Golgotha. Huyo ni Uzao wa Ibrahimu, Huyo hapo Adamu wa pili anaenda.

150 Katika bustani ya Edeni wakati Mungu alipokuwa, kwa utakatifu Wake, na mwaminifu kwa Neno Lake, wakati Hawa na Adamu walipokuwa wametenda uovu, wakati Mungu, Mwenyewe, akikimbia huku na huko kupitia bustanini, akipaza sauti, "Adamu, Adamu, uko wapi? Uko wapi, Adamu?" Kama mtu anataka kujua ni wapi. . .Mtu huyu alikuwa ni nani, Yesu, alikuwa ni Nani Yeye aliyekuwa akija kumtafuta mwanawe wa kwanza aliyepotea? Je, Mungu alimtuma Malaika? Alikuja Mwenyewe, alikuja Mwenyewe, hivyo ndivyo alivyokuja. Mnataka kuchukua. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

151 . . .haki. Kama hakuna haki, hakuna sheria. Kama huna haki. . .hukumu ya kuambatana nayo, hakuna haja ya kuwa na sheria. Kuna faida gani kuwa na sheria inayosema, faini ya dola kumi ukiipita taa ya kusimamisha, halafu usininii. . . kusema, "Usiipite taa ya kusimamisha," wala hakuna faini nyuma yake, hakuna adhabu ya kulipa, hakuna hukumu? Bila hukumu, hakuna haki. Kwa hiyo haki ilikuwa ni kufa, kwa hiyo lilikuwa ndilo jambo pekee angaliweza kufanya.

152 Ndipo basi alipomwona Hawa amesimama pale, maskini mwanamke huyo mrembo, huyo mwanamume halisi aliyesimama pale, hiyo misuli mikubwa, migumu, na damu ikitiririkia mikononi mwake kutoka kwenye hiyo ngozi ya kondoo iliyolowa damu, maskini Hawa akisimama pale, mwanamke mrembo kuliko wote aliyewahi kuwako ulimwenguni, kwa sababu aliumbwa kwa mkono wa Mungu Mwenyewe, macho yake yalikuwa kama nyota za mbinguni. Hakuhitaji vipodozi vya Max Factor kumfanya mrembo, na wakati alipokuwa, huku namna *hii*, naye huyo hapo amesimama pale, damu ikitiririkia maskini mwili wake wa kupendeza, amesimama hapo, akiuangalia uso wa Mungu, katika Nuru hiyo kuu, ametundikwa hapo kwenye mitende hiyo, "Ondoka Mbele Zangu."

153 Sasa, mwangalieni Adamu anapoanza kuondoka, na miguuni mwake maskini hizo ngozi za kondoo zilizolowa damu, zikipigapiga namna *hiyo* miguuni mwake, asingeweza kuvumilia hilo, Yeye ni Baba, kasema, "Hebu kidogo, nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka."

154 Ilikuwa wapi? Hii hapa pale Kalvari. Huyu hapa anapanda juu, huyu Adamu wa pili, Mungu Mwenyewe alishuka na kufanyika mtu, akipanda juu ya kilima.

155 Ibilisi daima alilichukia Neno hilo, lakini hiyo ni kweli. Naam, bwana. Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii. Watu siku hizi

walio na dini hii ya kijamii, wakisema ya kwamba Yesu, "Mtu mzuri tu, mwa—mwanafalsafa, ni vizuri kusikia mafundisho yake."

156 Kama Yeye hakuwa Mungu, kama hiyo haikuwa ni Damu ya Imanueli, basi Yeye alikuwa ni mwanadamu kama nilivyo mimi, hiyo ni kweli, nasi tumepotea. Alikuwa Mungu. Mungu, Roho Mtakatifu, alimtia uvuli Mariamu na kuumba Seli ya Damu iliyozaa, si damu ya Kiyahudi, si damu ya Mataifa, bali Damu ya Mungu Mwenyewe. Damu hutoka kwa jinsia ya kiume, hii ni Damu iliyoumbwa, hakuna kujuana kimwili ndani yake hata kidogo. Na huyo alikuwa ni Mungu Mwenyewe, akienda, akipanda kilima pale.

157 Hebu tumwangalie Yeye, alikuwa amejizungushia joho dogo mabegani Mwake, lilikuwa limefumwa kote bila mshono. Ninaona wakati akitembea, ninamwangalia kwa imani, nikiwaonyesha ninyi nyote Yeye kwa imani, kuna vitone vidogo vyekundu vilivyojaa nyuma ya koti hilo. Ni kitu gani kinachofanya hilo namna hiyo? Anapopanda juu zaidi barabarani, huku msalaba ukisugua begani mwake, ninaona hivyo vitone vikianza kuwa vikubwa zaidi na zaidi. Hivyo ni nini? Kuna nini? Mara vyote vinakuwa mrusho mmoja mkubwa mno, wa damu. Ndipo ninasikia kitu kingine kikipigapiga mguuni Mwake, Adamu wa pili, akipanda mlimani huku vazi lililolowa damu likiupiga mguu Wake.

158 Mnajua, Shetani alisema, akaangalia kote, kasema, "Unajua nini? Hata siamini yeye ni nabii sasa. Ninajua huyo hawezi kuwa ni Mungu, Mungu kamwe asingetenda hivyo, kuacha kundi hilo la walevi wenye dhihaka wamrarue namna hiyo, kuwaacha wamwite *mtakatifu anayejibingirisha*," ninazungumza nawe, "kuwaacha wamwite *wa mtindo wa kale*, kitu kama hicho, 'Wewe ni maskini mlokole,' Yeye asingefanya hivyo kamwe."

159 Lakini ilikuwa . . . Yeye alikuwa ni Mungu. Ufalme Wake ulitoka juu, wajumbe Wake ni kitu kile kile, Ufalme wao uko juu, wanatenda kama kutoka *huko* juu, wanazungumza kuhusu juu *kule*, "Palipo na hazina yao, ndipo ilipo mioyo yao pia," wanazungumzia jambo hilo.

160 Anapopanda juu ya kilima, ninaweza kuona hayo mauti. Shetani alituma mwiba huo wa mauti kule, kasema, "Shuka uende ukamshike sasa." Kasema, "Shuka uende ukamshike, sasa ndio wakati wa kumshika."

161 Huyo nyuki, kama nyuki mkubwa wa mauti, akaanza kuvuma karibu Naye, akivuma huku na huko kumzunguka, asema, "Naam, mwangalieni akitokwa na damu, mwangalieni, mate usoni mwake mwote. Waangalieni wote wakicheka, wakimdhihaki."

162 Ninamwona maskini mwanamke mmoja akitoka mbio, na kusema, "Kwani alifanya nini? Amefanya uovu gani? Yeye

alifanya nini, ila kutuhubiria Injili? Alifanya nini, ila kuwaponya wagonjwa wenu?"

Mtu fulani anampiga kofi aondoke njiani, kasema, "Waweza kumsikiliza mwanamke huyo mwendawazimu badala ya kasisi wako? Kwea kilima pamoja naye."

163 Wakampiga tena, anapanda juu kilimani. Nyuki huyo anasema, "Nitamshika baada ya kitambo kidogo watakapomtundika msalabani."

164 Mnajua wadudu wote, nyuki na kadhalika, wana mwiba, na mauti ni nyuki, yana mwiba. Lakini mnajua nini? Wakati mmoja wa hao nyuki anapowahi kudunga mwiba wake ndani kabisa, anauchomoa mwiba wake. Ndugu, wakati alipouchomeka mwiba wake katika mwili huo, huyo hakuwa mwanadamu, Yeye alitia mwili wake nanga katika Imanueli, na alipofanya hivyo, Yeye aliuchomoa mwiba wake. Ninawaambia, kwa Uzao wa Ibrahimu sasa, yeye anaweza kuvuma na kutoa sauti, bali hawezi kuwa na mwiba wowote.

165 Mmoja wao akikaribia kufa alisema, "Ee mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi, kwa Bwana wetu Yesu Kristo!"

166 Naam, anaweza kuvuma, na kutoa kelele nyingi, na kuzozana, na kuvuta hospitali, ndani, yako, hospitali, na kuwaambia madaktari wanaosimama pale, na lundo la kuomboleza na kulia, lakini unamwangalia usoni na kusema, "Ewe mauti, u wapi mwiba wako? Ninaweza kuelekeza kidole kule aliko Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, ambaye nilizaliwa kwa Damu Yake, Yeye aliuchomoa mwiba huo kutoka kwenye mauti, kwa hiyo, ewe mauti, huna mwiba kwangu."

Ewe kaburi, "Nitakufinyanga siku moja."

167 "U wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi, kwa Bwana wetu Yesu Kristo." Na Uzao Wake utamiliki malango ya maadui zake, utamiliki lango la maadui zake wote.

168 Naye alipokuja, alimiliki kila lango, lango a magonjwa, lango la mauti, lango la kuzimu, lango la majaribu, lango la kaburi, Yeye alimiliki kila lango na anatupatia bure, na kutufanya zaidi ya washindi kwa Yeye aliyetupenda, na kujitoa Mwenyewe kwa ajili yetu.

169 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu tunapowazia hilo. Nashangaa usiku wa leo, kama kwa bahati: Ni wangapi walio katika jengo hili hapa ambao hawamjui Yeye kama Mwokozi wenu, nawe unajua ya kwamba maisha yako hayako sawa na Mungu, waweza kuinua mkono wako? Useme, "Niombee, Ndugu Branham, katika maombi haya ya kumalizia, nataka uniombee."

170 Mungu akubariki, huko nyuma pembeni. Mungu akubariki huko nyuma kabisa, mama. Kunaweza kuwako na wengine zaidi? Ni wangapi zaidi, huko juu kwenye roshani? Je, ninaweza kuona mikono fulani huko juu? Hao watu wote, Mungu awabariki huko nyuma. Mungu akubariki hapa, mama.

171 Je, mtu mwingine ungeinua tu mkono wako? Haitakudhuru. Jamani, inua tu mkono wako, useme “Mimi. . . ” Unajijua mwenyewe. Wasema, “Ndugu Branham, mimi si Uzao wa Ibrahimu, mimi ni mfuasi wa kanisa.” Mungu akubariki hapa, bwana. “Mi—mimi si Uzao wa Ibrahimu.” Mungu akubariki, mama, papa hapa. Bwana awaneemeshe, usiku wa leo. Huko upande wangu wa kulia, naam, Bwana awabariki.

172 Mtu mwingine? Sema, inua mkono wako, na uinue tu mkono wako, useme, “Nikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi yako, ninataka ku—nataka kuwa Uzao wa Ibrahimu.” Kwa sababu kumbuka, kama wewe si Uzao wa Ibrahimu, huko katika ahadi.

173 Sasa, huenda ukawa mfuasi wa kanisa fulani, na hilo ni sawa. Naam, bwana. Sina neno dhidi yako kuwa mfuasi wa kanisa, nafikiri hilo ni jambo jema. Lakini, ndugu, dada, hilo halitakusaidia hata kidogo saa ya kufa kwako, ama katika Kuja kwa Bwana Yesu, Itakubidi kuwa Uzao wa Ibrahimu.

174 Na njia pekee unayoweza kuwa Uzao wa Ibrahimu ni kujikana mwenyewe, na kufa kwa nafsi yako mwenyewe, na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, kwa sababu Uhai uliokuwa ndani ya Kristo unatufanya Uzao wa Ibrahimu. Tunachukua Uzao wake kwa Roho Mtakatifu tuliyepewa kwa ahadi ya Mungu, “Na ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

175 Mikono minane ama kumi imeinuliwa. Je, kunaweza kuwako na wengine kwa uaminifu mnyofu? Kuwa mwaminifu tu kwako mwenyewe. Kama wewe ni mfuasi wa kanisa, hatukuombi uje ujiunge na kanisa hili, la, tunataka tu uwe Uzao wa Ibrahimu.

176 Ndugu, dada, huenda nisiwaone tena katika maisha haya, lakini kule kwenye ile Hukumu, itanibidi kuwakabili. Mnaona? Sasa, kumbukeni usiku huu, tarehe 13 Februari, 1961, wakati siku hii itakapofingirishwa kule kwenye turubai ya anga za Hukumu, mtaukumbuka mkutano huu.

177 Mungu akubariki hapo ukutani hapo. “Ninataka kumwamini Yesu, nataka kuwa Uzao wa Ibrahimu, usiku wa leo.” Nilinunua. . .Biblia ilisema aliye kwa nje si Myahudi, bali yule aliye kwa ndani. Uzao wa—wake utamiliki malango ya adui.

178 Tumemtimua adui sasa. Mikono kumi au kumi na miwili tayari imeinuliwa. Hiyo. . .Tunaonyesha ya kwamba tumemweka adui mbioni. Je, kunaweza kuwa na mwingine

atakayejiunga nasi usiku wa leo, na kuinua mikono yako na kusema...? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Je, kunaweza kuwako, huko nyuma? Mungu akubariki huko nyuma. Naam, ndugu yangu, huko juu kwenye roshani, Bwana akubariki. Naam. Jiunge na safu zetu. Tumemfanya adui kutimua mbio sasa.

179 Jana usiku tulimfanya aanze kuwatoroka wagonjwa. Angalieni tu hao wagonjwa wa kansa, na wote, waliokombolewa hapa jana usiku. Adui anaondoka sasa. Juma lililopita tulipigana tu, na kukatakata, na kila kitu tulichoweza, lakini tukamfanya adui kuondoka. Mnaona?

180 Sasa, wengi wanakuja huku, wakija katika safu, wakichukua...wanaingia moja kwa moja. Kuna...Hivi hutakuja ujiunge nasi, usiku wa leo? Unganisha mikono yako na Mungu usiku wa leo, uyafie mambo ya ulimwengu na umkubali Kristo kama Mwokozi wako. Je, utainua mkono wako kabla hatujaomba? Useme, "Nikumbuke." Mungu akubariki huko nyuma kabisa, ninaweza kuona mkono wako umeinuliwa huko nyuma kabisa. Mwingine tu?

181 Vipi kuhusu mtu aliye karibu hapa, asiye Mkristo? Useme, "Ninataka, unikumbuke, Ndugu Branham. Niombee tu wakati ukiomba, nikumbuke tu katika maombi yako." Nitafanya hivyo. Vema. Sasa hebu na tuendelee kuinamisha vichwa vyetu.

182 Sasa, Baba wa Mbinguni, hakuna mmoja wetu anayejua ya kwamba tutakuwa hapa kesho, huu huenda ukawa ndio usiku wa mwisho duniani tunaotumia. Kuna siku moja nitakayoifunga Biblia hii kwa mara ya mwisho, wakati fulani nitafunga macho yangu, na kuinamisha kichwa changu kwa mara ya mwisho, na kila mtu hapa ndani atafanya vivyo hivyo. Hatujui wakati huo utakuja lini, Bwana. Tunajua kuna chumba kikubwa mno, chenye giza, kilichowekwa mbele ya kila mmoja wetu, kila mwanadamu, kinaitwa *mauti*.

183 Na tunapowazia juu ya yule mwandishi wa *Thanatopsisi*, kila wakati moyo wangu unapopiga, tunafikia pigo moja karibu na chumba hicho. Kila wakati moyo wangu unapopiga, na saa hiyo inapiga, tunakaribia tu kwa pigo moja zaidi, siku moja utafikia pigo lake la mwisho.

184 Mungu, hatutaki, ninasihi kwa ajili ya watu hawa, hatutaki kuingia kwenye chumba hicho tukipiga mayowe, na kulia, na kutamani maisha zaidi, na dakika chache za kutubu. Mungu, tunataka kuingia humo kwa ujasiri. Tutaingia humo kama Uzao wa Ibrahimu, ile ahadi mioyoni mwetu, tukijua jambo hili, kwamba tunamjua Yeye katika nguvu za kufufuka Kwake, kwamba siku moja, atakapoita, tutatoka katika wafu na kufufuka, na kwenda kuwa pamoja Naye, tupate kuwa pamoja Naye daima.

185 Ninawaombea hawa walioinua mikono yao, Bwana. Wengi waliinua mikono yao, wao ni waaminifu, Mungu. Ha—hawakufanya hivyo kwa nguvu zao wenyewe, ilibidi kuwe na nguvu walizopewa, na hizo zilikuwa ni nguvu Zako. Nao wakainua mikono yao kwamba walikuwa waaminifu katika hilo.

186 Mungu, imeandikwa katika Neno ya kwamba kuomba kwake mwenye haki, kwa bidii. . .Sasa, hakuna mmoja wetu aliye mwenye haki, bali tunaikubali haki Yake, nasi tunaileta Damu Yake mbele Zako, tunaleta Neno Lake mbele Zako, kama Yeye alivyosema, "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya."

187 Sasa, tunakuletea watu hawa, kwa imani, moja kwa moja mbele Zako, Bwana. Hao hapo, wametenda dhambi, wamefanya makosa, wanataka msamaha wa dhambi yao. Waliinua mikono yao Kwako kwamba, na ili niwaombee kwamba wanasikitika kwamba walifanya hivyo. Bwana Yesu, wasamehe. Jalia wapate ile amani tamu halisi ipitayo ufahamu. Wakielewa ya kwamba Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe, ili—ili wapate ujasiri wa kuinua mkono wao.

188 Pia jalia wawe na ufahamu huu, pia, Bwana, kwamba walichaguliwa, la sivyo wasingeweza kamwe kuinua mkono wao, kwa maana Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Jalia wajue ya kwamba Mungu, Baba, amesimama kando yao, akinena na moyo wao, nao wamefanya chaguo hili.

189 Pia alisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, amepita kutoka mautini kuingia Uzimani, wala hataingia Hukumuni, bali tayari amepita kutoka mautini kuingia Uzimani," anao Uzima wa Milele sasa. Baba Mungu, usingemkataa hata mmoja.

190 Nami naomba ya kwamba utawarehemu hawa. Nami ninaomba ya kwamba utawasaidia, na kuwapa ujasiri sasa, baada ya kunukuu Maandiko haya, kwamba Wewe ndiwe uliyewafanya wainue mkono wao, kwa kuwa Wewe ulisema hivyo, "Hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba watakuja." Na hebu wajue, juu ya maungamo hayo papo hapo inathibitisha ya kwamba Wewe unawasamehe dhambi yao.

191 Sasa, jalia wasilionee haya, jalia wasimame kwa ujasiri, waseme, "Naam, sasa ninalikubali juu ya msingi wa Neno Lake, ya kwamba kamwe sitaingia kwenye Hukumu ya waliohukumiwa, kwa sababu Mungu alisema na moyo wangu, nami nikainua mkono wangu kwamba ningemkubali kama Mwokozi wangu. Nilitaka kukumbukwa katika maombi." Tujalie, Baba.

192 Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, naomba kila mmoja aliyeinua mkono wake, kama mnaamini ninayowaambia, enyi Wakristo, ombeni, Mungu alisema hivi: Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza," sasa, ni kitu gani kilichokufanya uinue mkono wako? Ni Roho Mtakatifu pale akikwambia, akikushawishi ya kwamba umekosea. "Na wote alionipa Baba," ama alionena nao, "watakuja," (Nawe ulifanya hivyo, ukainua mkono wako, "Mimi ni mwenye dhambi, ninataka msamaha, nilikosea.") "Sitamtupa nje kamwe, nitampa Uzima wa Milele, nimfufue siku ya mwisho."

193 Sasa, kuna jambo moja zaidi ninalowataka mfanye, "Yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu." Sasa, ninawaomba mfanye jambo moja katika wema wa Mungu. Wazia tu jinsi alivyokuwa mwema kukuacha uinue mkono wako.

194 Nilizungumza na msichana mdogo nilipokuwa bado ni mhubiri wa Kibaptisti, nilikuwa huko chini Nashville, Tennessee, nami nikajisikia kuongozwa kumwambia ya kwamba niliamini Mungu alikuwa akimpa wito wa mwisho. Akakutana nami nje ya kanisa usiku huo, naye akasema, "Usiwahi kuniaibisha namna hiyo tena!"

Nikasema, "Sikukuaibisha kamwe, natumaini sikukuaibisha." Alikuwa binti ya shemasi.

Akasema, "Mimi ni kijana, nami nina wakati mwingi sana wa kufanya hilo."

195 Nikasema, "Mama, kamwe nisingekuelekezea kidole changu kama sikuhisi kwamba ilikuwa ni sawa. Kamwe sikufanya wito wa madhabahuni kama sikuwazia . . . " Naye akanikemea vibaya sana.

196 Yapata miaka miwili baadaye, nilikuwa kule chini pamoja na rafiki yangu wa zamani, Ndugu Morrison, kanisa la Kibaptisti, kufanya mkutano mwingine, na nilipofanya hivyo, nilitembea mtaani, naye alikuwa msichana mzuri, alikuwa akitembea mtaani, imekuwa ni miaka ishirini na mitano iliyopita, huku sketi zake za ndani zimening'inia chini. Loo, jinsi alivyoonekana wa kuchukiza! Nikawaza, "Huyo hawezi kuwa ni binti wa huyo shemasi!" Naye akaniangalia kwa makini, kwa namna fulani akatabasamu, akageuza kichwa chake upande. Nikasogea karibu naye.

Akasema, "Halo, Mhubiri."

Nikasema, "U hali gani?"

Akasimama pale pembeni kidogo, kasema, "Njoo, twende pamoja chumbani mwangu."

Nikasema, "Asante, kidogo nina haraka."

Akaingiza mkono kwenye pochi lake, akasema, "Ungetaka sigara?"

Nikasema, "Sasa, hivi huoni aibu kusema hivyo?"

Akasema, "Labda ungekunywa pombe pamoja nami. Nitailipia kama utainywa."

197 Nikasema, "Jionee aibu, mama! Hivi hujionei aibu kumwomba mtumishi wa Kristo kitu kama hicho?" Nikaanza kuondoka, nikasema, "Nitakuwa nikikuombea."

Akasema, "Hebu kidogo, hakuna haja."

Nikasema, "Kwa nini?"

Akasema, "Unakumbuka usiku ule tukisimama pale karibu na kile kichaka cha waridi, kando ya lile kanisa la Kibaptisti?"

Nami nikasema, "Naam."

198 Kasema, "Baba yangu angali ni shemasi kule." Kasema, "Unaweza kusimulia hili popote utakapo, popote uendapo, ukitaka." Akasema, "Huo ulikuwa ndio wito wangu wa mwisho." Akasema, "Unajua, tangu wakati huo," kasema, "sikuzote nilikuwa nikisikia wito moyoni mwangu kumjia Mungu," akasema, "lakini tangu wakati huo," akasema, "nimekuwa mgumu zaidi na zaidi."

199 Sasa, hili ndilo tamshi alilotoa huyo msichana: Akasema, "Moyo wangu ni mgumu sana dhidi ya Mungu, na dhidi ya kanisa, na kila kitu," kasema, "ningeweza kuiona nafsi ya mama yangu ikikaangwa kuzimuni kama chapati maji na kuicheka." Mnaona?

200 Sasa Yeye amekurehemu. Alibisha moyoni mwako, nawe ukainua mkono wako, "Naam, Bwana, nimekosea." Huyo alikuwa ni Baba. Sasa utamkiri vya kutosha, waweza kusimama tu kwa miguu yako? Sitakuomba ufanye jambo lingine, simama tu kwa miguu yako ili watu waweze kuona ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu aliyebisha moyoni mwako. Sasa, kumbukeni, watoto halisi, wa kweli, "Mungu alibisha moyoni mwangu, ninataka kusimama kwa miguu yangu, kuwafanya tu watu wajue."

201 Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ewe kijana. Mtu mwingine asimame. Hiyo ni kweli. Wote waliobisha, "Sasa naamini," simameni tu kwa dakika moja, kwa muda kidogo tu. Tafadhali, simameni tu kwa dakika moja, kila mmoja. Hilo ni sawa. Kunaweza kuwa na mwingine anayetaka kusimama, wakati huu tu? Sema, "Alibisha moyoni mwangu, sikuinua mkono wangu, bali nitamsimamia sasa hivi, nitasimama sasa hivi. Ninaamini nitamsimamia sasa hivi, kwa sababu Yeye alibisha moyoni mwangu, sitaki moyo wangu kamwe uingie katika hali hiyo mbaya namna hiyo. Wakati ungali mwororo, nitasimama."

202 Sasa, ninawaambia jambo hili kwa mamlaka ya Neno la Mungu: Kama ukimtetea hapa, Yeye atakutetea kwenye Hukumu, "Yeye anayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu."

203 Ningependa kuwauliza ninyi watu, ninyi Wakristo wapendwa ambao sasa hivi mmekuwa Wakristo katika Kristo, ndio kwanza mpate mwa—mwaliko wa kuwa Uzao wa Ibrahimu, tafuteni kanisa zuri na mkabatizwe. Mungu akubariki, Dada, kwa kusimama namna hiyo. Hilo ni zuri sana.

204 Sasa, endeleeni tu kusimama, ninataka kuwaombea tena. Na mtafute kanisa zuri, mkabatizwe katika ubatizo wa Kikristo, na mtafute ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kuna vijana wanaosimama, vijana wanaume, na, wangekuwa wahudumu na wamishenari, Mungu ayabariki Maisha yenu ya kifalme.

205 Sasa, ninyi ambao mmeinamisha vichwa vyenu, ninawatakeni mfungue macho yenu, kisha mgeuke na kuangalia, mwone ni nani. Nami ninawatakeni sasa, tunaposimama, kuwapa mkono wa kuume wa ushirika, kama waaminio Wakristo, mseme, "Karibuni." Waalikeni kanisani mwenu, ama kitu fulani. Sasa, hebu sote na tusimame kwa miguu yetu. Huku mkipeana mikono nao, semeni, "Karibu katika Ufalme wa Mungu, usiku wa leo," semeni, "ndugu yangu msafiri aliyebarikiwa," geukeni, kila mmoja wenu, peaneni mikono na watu hao sasa tunapoimba.

> Jinsi tu nilivyo, bila hata ombi moja,
> Ila kwamba ninii Yako . . .(Jambo ndilo hilo, Wakristo, iweni wazuri sana.)
> . . .ilimwagwa kwa ajili ya . . .(Ninaangalia juu kwenye roshani, vijana wakilia, watu wakitetemeka.)
> . . .kwamba Wewe umeniamuru nije Kwako;
> Ee Mwana-Kondoo . . .na . . .

206 Ndugu Buntain anasema kuna chumba cha maombi kwenye orofa ya chini. Unakifikiaje, Ndugu? Moja kwa moja tu kupitia malangoni, kama ungetaka kushuka, katika dakika moja tu. Nami nitamrudishia ibada. Na labda baadhi yenu hamjaninii . . . Ni wangapi ambao hawajapata ubatizo wa Roho Mtakatifu? Inua mkono wako, na unatafuta. Unataka kuwa . . .Mungu awabariki. "Yeyote atakaye, na aje." Hiyo ni kweli?

207 Sasa, hivi hamna furaha, ninyi ambao mmesimama na kumkiri Kristo, usiku wa leo? Kama unajisikia vizuri sana kulihusu moyoni mwako, inua mkono wako kusudi watu waone, wewe uliyeinua mkono wako, wewe uliyekuja. Angalieni pale, kila mmoja wao, asilimia mia moja. Naam, bwana. Jambo ndilo hilo. Ni wangapi wenu ninyi nyote mnafurahia kwamba ninyi ni Wakristo, usiku wa leo? Inua mkono wako.

208 Biblia ilisema nini? Uzao Wake utamiliki lango la adui. Amina. Tulishinda usiku wa leo katika Kristo, Mshindi wetu mkuu. Tulibomoa kuta za dhambi, tukabomoa kuta za kutojali, na nafsi zikaingia katika Ufalme wa Mungu zipate kufufuka katika ufufuo katika siku ya mwisho. Hivi hatuna furaha?

Vema, Dada, "Nampenda, nampenda, kwani alinipenda kwanza." Kila mtu sasa, sote pamoja:

> . . . mpenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

209 Loo, hivi hamumpendi? Sasa, msiondoke sasa, nataka mnifanyie jambo fulani. Sasa, tunapouimba tena, ninawatakeni mpeane mikono na mtu aliye mbele yenu, mtu aliye nyuma yenu, kulia na kushoto, na kusema, "Mungu akubariki, ndugu msafiri, ama dada. Nina furaha kuwa hapa katika nyumba ya Mungu pamoja nawe." Hebu na tufanye hivyo sasa tunapoimba.

> Na . . . (Mungu akubariki, ndugu yangu msafiri. Mungu akubariki, ndugu yangu msafiri. Mungu akubariki, ndugu yangu.)
> . . . alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Juu ya ninii ya Kalvari . . .

Sasa hebu na tumwimbie huo tunapomwinulia mikono yetu.

> Na . . .

Inueni mikono yenu.

> . . . mpenda . . .

Ninawakabidhi kwa mchungaji wenu.

61-0213 Na Uzao Wako Utamiliki Mlango Wa Adui Zake
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org